# Nipashe

MWANGA WA JAMII

Jumamosi Juni 29, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579957

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper




UKURASA 13



## Mwili wakutwa kichakani umekatwa miguu, mkono

UKURASA 3

# Tundu Lissu basi tena



**SPIKA** Ndugai atangaza amepoteza ubunge, aweka bayana sababu za kuvuliwa kwake...*Endelea uk. 3*

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**MAHAKAMA YAMALIZA MGOGORO WA MAZISHI**

BAADA ya mvutano wa wiki mbili, hatimaye Mahakama ya Wilaya ya Mwanga, imeupa upande wa ndugu wa marehemu, haki ya kuuzika mwili wake...

UKURASA WA 4

**KIZIMBANI KWA TUHUMA KUTAKATISHA MIL. 967.6/-**

RAIA wa China, Yu Peishan (44), amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, akikabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi, ikiwamo ...

UKURASA WA 5

**AFARIKI AKIZUIA LORI KWA GOGO**

MKAZI wa Mtwara, Azizi Natende (33), amefariki dunia kwa kukanyagwa na lori alilokuwa anajaribu kulizuia kwa gogo baada ya kushindwa...



Rais Dk. John Pombe Magufuli akipokea zawadi ya picha ya kuchora toka kwa Mwenyekiti wa Jukwaa la Wabunge wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), Veronica Nataniel Macamo Dlhovo, baada ya mazungumzo Ikulu, jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Spika wa Bunge, Job Ndugai (wa pili kulia) na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Damas Ndumbaro. **PICHA: IKULU**

## Watanzania 9 wauawa kwa risasi Msumbiji

UKURASA 8

# CAG afunguka kodi kwa mtutu

**ATOA** ushauri kuweka mazingira rafiki, Utouh naye atema ya moyoni ... *Endelea ukurasa wa 2*

**MICHEZO** MAKONDA AMWANGUKIA MAGUFULI KIPIGO STARS UK. 31

MAONI, KATUNI UK.6

## Mahakama yamaliza mgogoro wa mazishi

**Na Mary Mosha,** MWANGA

BAADA ya mvutano wa wiki mbili, hatimaye Mahakama ya Wilaya ya Mwanga, imeupa upande wa ndugu wa marehemu, Kapteni mstaafu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Hussein Seushi, haki ya kuuzika mwili wake kwa imani ya dini ya Kiislamu.

Akisoma uamuzi juu ya shauri hilo mahakamani hapo jana, Hakimu Mkazi Mariam Lusewa alisema baada ya kupitia hoja za pande zote mbili, amempa haki ya mke wa marehemu na watoto wake sita kushiriki katika mazishi hayo kwa gharama zao lakini wajiepushe na vurugu zozote.

Alitoa uamuzi huo baada ya mke wa marehemu kushindwa kuthibitisha kwa nyaraka jinsi mumewe alivyohama kutoka kwenye Uislamu kwenda Ukristo kama wanavyodai.

Hukumu hiyo, ilitolewa siku 14 tangu kufariki dunia kwa Kapteni Seushi Juni 17, mwaka huu, huku familia ikichimba kaburi nyumbani kwake Kifaru, Mwanga na mazishi kuzuiwa na mwili kurejeshwa kwa ajili ya kuhifadhiwa katika Hospitali ya Rufani ya KCMC, Moshi, kusubiri kumalizika kwa kesi iliyofunguliwa na ndugu wa marehemu waliyoiomba mahakama kuwapa idhini ya kumzika ndugu yao kwa imani ya Kiislamu.

Hakimu Lusewa alisema pamoja na kwamba ni haki ya kila raia kuhama dini aitakayo, haiondoi kuwapo kwa utaratibu wa kuwa na nyaraka za dini husika kuonyesha mtu anavyohama dini moja kwenda nyingine.

Alisema amezingatia ukweli ambao haubishaniwi na pande zote kwamba Seushi alikuwa muumini wa dini ya Kiislamu na alidumu katika dini hiyo kwa takribani miaka 30 na alijaliwa kufunga ndoa na kupata watoto sita akiwa kwenye imani yake hiyo na hakuna ushahidi kwamba ndoa hiyo iliwahi kuvunjika hadi kufariki Juni 17, mwaka huu.

Wakili wa ndugu wa marehemu, Caessar Shayo aliomba mahakama kukubali maombi manne ingawa yalikubalika matatu likiwamo la kuruhusiwa kuzika kwa dini ya kiislamu.

Alidai kuwa mke wa marehemu na wanawe sita wameshindwa kuithibitishia mahakama kuwa ni madhehebu gani ambayo Seushi alihamia kama walivyodai hali ambayo imeleta kigugumizi.

Aliomba mahakama itupilie mbali hoja za familia ya marehemu ambayo inatamka kuwa wao ni Wakristo bila kutaja dhehebu na utaratibu uliotumika.

# CAG afunguka kodi kwa mtutu

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, ameishauri serikali kuweka kiwango cha kodi ambacho kitawafanya wafanyabiashara nchini kulipa kodi zao bila shuruti.

Hivi karibuni, maofisa wa Mamlaka ya Mapato (TRA) waliripotiwa kutumia askari wenye bunduki kudai kodi kwa wafanyabiashara jijini Arusha.

Wakati Prof. Assad akitoa rai hiyo, mtangulizi wake katika ofisi hiyo, Ludovick Utouh, ameshauri Watanzania kuwa wazalendo kwa kulipa kodi stahiki ili serikali ikusanye mapato mengi na kutekeleza miradi muhimu ya maendeleo.

Prof. Assad na Utouh walitoa ushauri huo jana jijini Dodoma wakati wa uzinduzi wa ripoti ya uwajibikaji ya mwaka 2017/18 inayohusisha mamlaka ya serikali za mitaa na miradi ya maendeleo, serikali kuu na mashirika ya umma pamoja na ufanisi, rushwa na ubadhirifu.

Ripoti hizo zimeandaliwa na Taasisi Fikra ya Uwajibikaji wa Umma (Wajibu) inayoongozwa na Utouh.

Akizungumza katika uzinduzi huo, Prof. Assad alisema: "Kodi inayokusanywa ni zao la vitu viwili ambavyo ni kiwango cha kodi na kiasi ambacho mfanyabiashara amekipata, yaani ile' tax base' (kiwango cha rasilimali) yenyewe. Ukiwa na kiwango cha kodi cha sifuri, serikali haiwezi kukusanya kitu.

"Lakini vilevile, ukiwa na kiwango cha kodi cha asilimia 100, wafanyabiashara hawawezi kufanya biashara kwa sababu hakuna 'incentive' (kichocheo) ya kufanya biashara, kwa hiyo katikati ya sifuri na 100, kuna kiwango ambacho ni kizuri zaidi.

"Sasa, mimi rai yangu ni kwamba tuweke kiwango ambacho kitawafanya wafanyabiashara waweze kulipa kodi zao bila shuruti. Tuwe tuna kiwango kizuri na tuwaelimishe wafanyabiashara wetu na watu wote wanaotakiwa kulipa kodi, walipe kodi zao bila shuruti kwa sababu kama 'rate' (kiwango) ni nzuri, inawafanya watu walete taarifa zao na walipe kodi."

Kuhusu uwajibikaji, Prof. Assad alisema ni neno ambalo msingi wake ni neno la Kiingereza 'account' ambalo maana yake ni mtu kutoa taarifa juu ya yale aliyoyafanya kwa mtu ambaye anahitaji hiyo taarifa na kwamba huo ndiyo msingi wa uwajibikaji.

Alisisitiza kuwa ili kuongeza uwajibikaji, kunahitajika taasisi imara za umma ambazo ni za usimamizi na uchunguzi na misingi mizuri.

"Ukishapata kitu hicho kama kipo, unahitaji eneo la pili kama taasisi za kijamii, nazo hizi ni lazima ziwe nzuri, zenye watu wenye uwezo ili uweze kufanya kazi zake sawasawa.

"Tukipata vitu hivi viwili, yaani hizi taasisi za kijamii zinaweza kupiga kelele pale ambapo taasisi za serikali haziwezi, basi mambo yanakwenda vizuri zaidi," Prof. Assad alisema.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa Wajibu, Utouh, alisema: "Wajibu tunaangalia zile ripoti za CAG, ni

INAENDELEA UK. 8



Baadhi ya watalii kutoka nchi ya Uingereza wakivutiwa na chemchemu ya maji ya moto, walipotembelea katika Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Mbaroni tuhuma mauaji aliyesamehewa na JPM

**Na Said Hamdani,** LINDI

JESHI la Polisi wilayani Kilwa mkoani Lindi linawashikilia watu watano kwa tuhuma za mauaji ya mkazi wa Mtaa wa Ukote, Kata ya Kivinje wilayani humo, Salum Chilima (32).

Watano hao wanadaiwa kumuua Chilima usiku wa Juni 22, mwaka huu kwenye klabu ya pombe za kienyeji eneo la Mtaa wa Kisangi, Kata ya Kivinje.

Kamanda wa Polisi mkoani Lindi, Pudensiana Protasi, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kueleza kuwa watu watano wanashikilia na jeshi hilo kwa mahojiano kuhusiana na mauaji hayo.

Aliwataja wanaoshikiliwa kuwa ni wahudumu wa klabu hiyo, Hadija Milanzi (49), Pilli Isumaili (35), Christina Diera (22), Elena Likama (43) na Hadini Mohamedi (54) ambaye ni mlinzi katika klabu hiyo.

Kamanda Protasi alibainisha kuwa marehemu Chilima aliwahi kuhukumiwa kutumikia kifungo cha miaka mitatu katika Gereza la Ligula mkoani Mtwara kwa kosa la kujihusisha na wizi na aliachiwa huru kwa msamaha wa Rais John Magufuli hivi karibuni.

"Taarifa ya kifo cha huyu mtu tuliletewa na kaka yake, Ahamad Nonga, mvuvi na mkazi wa Mtaa wa Kisangi, Kata ya Kivinje," Kamanda Protasi alisema.

Alidai chanzo cha kifo cha Chilima ni kupigwa na kitu kizito kichwani na kuchomwa na kitu chenye ncha kali eneo la shingoni na kwenye taya la kushoto kulikosababisha kutokwa na damu nyingi na kupoteza uhai wake.

Kamanda Protas alisema wanaendelea kumtafuta mmiliki wa klabu ya pombe za kienyeji ili aunganishwe na wenzake kwa ajili ya mahojiano zaidi.

## HABARI KITAIFA



Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, wakipita jirani na Soko jipya la Afrika Sana, lililoko eneo la Kijitonyama Mpakani A, jijini humo jana, ambalo ujenzi wake unakaribia kukamilika na kuwafanya wafanyabiashara wa soko hilo, kufanyia shughuli zao katika mazingira mazuri tofauti na ilivyokuwa awali. **PICHA: JOHN BADI**

# Tundu Lissu apoteza ubunge

**Na Godfrey Mushi,**
DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, ametangaza kuwa Mbunge wa Singida Mashariki na Mnadhimu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Tundu Lissu, amepoteza kiti cha ubunge kuanzia jana.

Kiongozi huyo wa Bunge amesema Lissu ambaye kitaaluma ni mwanasheria, amepoteza nafasi hiyo baada ya kushindwa kujaza fomu za tamko la mali na madeni na kutohudhuria vikao vya chombo hicho bila kutoa taarifa kwa Spika kuhusu mahali aliko.

Akitangaza uamuzi huo bungeni jijini Dodoma jana, Spika Ndugai alisema: "Kwa mazingira hayo, Kifungu cha 37(3) cha Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) Sura ya 343 kinanitaka kumtaarifu Mwenyekiti wa NEC katika mazingira kama haya nini cha kufanya.

"Kwa sababu hizo mbili, moja kwa Spika kutokuwa na taarifa ya kimaandishi au vinginevyo ya alipo Tundu Lissu na kwa maana hiyo kutoonekana bungeni, lakini pia kwa kutotoa tamko la mali na madeni kinyume cha Ibara ya 71(g), napenda kuwafahamisha kuwa nimemwandikia Mwenyekiti wa NEC (Jaji Semistocles Kaijage) kuwa kiti cha ubunge cha Jimbo la Singida Mashariki kilichokuwa kinashikiliwa na Lissu kwa tiketi ya Chadema kiko wazi."

Spika Ndugai alitangaza hayo baada ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa kuahirisha Bunge.

"Mtakumbuka kwamba ndugu yetu Tundu Antipas Lissu tumekuwa hatupo naye hapa bungeni tangu Septemba 2017, kwa sababu ambazo zinafahamika na kila mtu, aliondoka hapa kwa ajili ya matibabu nchini Kenya.

"Kufanya hadithi iwe fupi, kwa zaidi ya mwaka mmoja uliopita hadi sasa, amekuwa akionekana katika vyombo mbalimbali vya habari vya kitaifa na kimataifa akitembelea nchi mbalimbali Marekani na Ulaya.

"Alikuwa akishiriki kwenye mikutano na kutoa mihadhara mbalimbali katika masuala mbalimbali, lakini kwa muda wote huo hajafika hapa bungeni na kwa muda wote huo, hajawahi kutoa taarifa yoyote ile kwa Spika kuhusu alipo na anaendeleaje.

"Wala hajawahi kuleta taarifa yoyote kwa kupitia hata kwa uongozi wake wa kambi au kwa chama chake hapa bungeni.

"Sasa kama mnavyojua katiba yetu iko wazi katika mambo ya aina hii na baadhi ya wabunge wameshapata matatizo, ninyi mnajua kutokana na utoro wa namna hii wa kushindwa hata kumwambia Spika niko mahali

INAENDELEA UK. 8

# Waziri atangaza kuifumua TBA

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, ametangaza kuufumua Wakala wa Majengo ya Serikali (TBA) kutokana na kusuasua kwa miradi inayotekelezwa na wakala huo.

Vilevile, waziri huyo amemwagiza Katibu Mkuu - Sekta ya Ujenzi kumpa majina ya wakala wasimamizi wa miradi ya TBA nchi nzima ili ajue taaluma.

Katika ziara yake kwenye mradi wa ujenzi wa nyumba za makazi unaoendelea Magomeni na Bunju jijini Dar es Salaam jana, waziri huyo alisema amebaini ujenzi wake umelala licha ya majengo hayo kutakiwa kukabidhiwa Desemba mwaka huu.

Alisema changamoto kubwa aliyobaini ni miradi hiyo kukabidhiwa kwa watu wenye taaluma nyingine na wasio na mipango.

"Majengo haya nimeambia yamekamilika kwa asilimia 40 tu, sijaridhishwa na kasi ya ujenzi wa mradi huu, nilichokibaini eneo hili halionekani kama kuna watu wanafanya kazi, limelala, nimeuliza watendaji wangu wananiambia limelala kwa sababu fedha hakuna," alisema.

"Huwezi kuingia mikataba na mtu akakuletea kokoto, simenti? Hivi simenti na kokoto tunalipa kama chumvi au mboga za mchicha? Tunaingia mkataba halafu fedha zinalipwa baadaye," alisema.

Kamwelwe aliongeza kuwa alitarajia eneo hilo akute watu wanaendelea na kazi ili ahadi iliyotolewa kwa Rais John Magufuli kwamba ifikapo Desemba, nyumba hizo ziwe tayari, itimie.

Kutokana na changamoto aliyoikuta, waziri huyo alitoa maelekezo kwa Katibu Mkuu - Sekta ya Ujenzi kuwabadilisha wafanyakazi

INAENDELEA UK. 8

# Mwili wakutwa kichakani umekatwa miguu, mkono

**Na Mohab Dominick,**
KAHAMA

MTU ambaye hajafahamika mara moja, amekutwa kichakani akiwa amefariki dunia huku baadhi ya viungo vyake vikiwa vimeondolewa.

Tukio hilo lilitokea katika kitongoji cha Nunga, Kata ya Ngogwa wilayani Kahama baada ya wananchi kuukuta mwili huo ukitoa harufu, huku viungo kama mkono, sehemu za siri na miguu vikiwa vimeondolewa na watu wasiojulikana wanaodaiwa kutekeleza mauaji hayo.

Ofisa Mtandaji wa Kata hiyo, Michael Magoyi, alisema jana kuwa tukio hilo, kutokana na hali ya mwili, limetokea siku za karibuni chini ya wiki moja na wananchi walipogundua walitoa taarifa kwa mwenyekiti wa kitongoji hicho.

"Taarifa ya kuokotwa kwa mwili huo nilizipata kwa mwenyekiti wa kitongoji cha Nuja ambaye alidai kwamba alipelekewa taarifa hizo na mwananchi aliyefahamika kwa jina la Thomas Shaban. Baada ya kupokea taarifa hizo, nilifika eneo la vichaka kisha nikapiga simu polisi ambao walifika haraka na kuokota kiwiliwili hicho.

Magoyi alisema tukio hilo limezua taharuki miongoni mwa wananchi hasa baada ya watu waliofanya uhalifu huo kukata viungo mbalimbali vya mwili wa mtu huyo kisha kutoweka navyo.

"Kwa kweli mwili ulikuwa umeharibika vibaya sana na kwamba viungo vyake vimekatwa katwa na kubaki kiuno, kifua, mkono mmoja na kichwa. Hatukuweza kusogea ili kujua ni jinsia gani na kwa hali hiyo

INAENDELEA UK. 8


**UBAPA COMPANY LIMITED AND TRIBUNAL BROKER**

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kwa idhini tuliyopewa na **CRDB tawi la Musoma** tutauza kwa njia ya mnada wa hadhara dhamana ya mdaiwa **ELIZABETH CYPRIAN MASIKU** nyumba iliyoko katika Manispaa ya Musoma.

**MDAIWA:** **ELIZABETH CYPRIAN MASIKU**
**JINA LA HATI-SACKIBU MOHAMED KABYEMELA**
**CT NO. 24373**
**LONO255478**
**FILE NO. MTC/4964**
**Plot No. 249 Block U HD Mutex area**
**Musoma Municipality**

**MASHARTI YA MNADA**
Mnunuzi atakayenunua nyumba hiyo baada ya nyundo ya dalali kutua anatakiwa kulipa 25% papo hapo au 100%. 75% italipwa ndani ya siku 14. Kushindwa kulipa 75% ndani ya siku 14 mnunuzi amepoteza **HAKI YAKE NA MNADA HUU UTARUDIWA TENA.**

**Kwa mawasiliano zaidi**
**Mkurugenzi: Juma Hasan Ebambo**
**Simu: 0753 338008**
**S.L.P 339 MUSOMA - MARA**

215301102

# Raia China apandishwa kizimbani tuhuma kutakatisha mil. 967.6/-

**Na Hellen Mwango**

RAIA wa China, Yu Peishan (44), amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, akikabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi, ikiwamo kughushi, kusababisha hasara na kutakatisha Sh. milioni 967.6.

Mshtakiwa huyo alisomewa mashtaka yake mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Augustine Rwizile.

Katika kumsomea mashtaka, upande wa Jamhuri uliongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Mkunde Mshanga, akisaidiana na Wakili wa Serikali, Glory Mwenda.

Mshanga alidai kuwa kati ya Agosti 7 na 15, mwaka jana jijini Dar es Salaam, kwa nia ya kulaghai na kudanganya, alighushi leseni ya Bodi ya Michezo ya Kubahatisha (GBT) yenye jina Agama Lotto and Mining Ltd, akionyesha kuwa imetolewa na bodi hiyo huku akijua si kweli.

Katika shtaka la pili, ilidaiwa kuwa Machi, 2017 jijini Dar es Salaam, mshtakiwa huyo alighushi leseni nyingine ya bodi hiyo yenye jina la Thinamy Entertainment kwa lengo la kuonyesha kuwa ni halali imetolewa na bodi hiyo.

Mshanga aliendelea kudai kuwa Oktoba 29, mwaka jana, jijini Dar es Salaam, mshtakiwa alighushi cheti cha kulipia kodi cha Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa lengo la kuonyesha ni halali na kimetolewa na mamlaka hiyo, huku akijua si kweli.

Ilidaiwa kuwa Januari, mwaka huu, mshtakiwa huyo alighushi mashine ya kodi ya michezo ya kubahatisha yenye jina Rong xin Investiment Co. Ltd kwa lengo la kuonyesha ni halali imetolewa na TRA huku akijua si kweli.

Katika shtaka lingine, ilidaiwa kati ya Agosti, mwaka jana na Mei 23, mwaka huu, jijini Dar es Salaam, mshtakiwa alishindwa kulipa kodi ya mashine za kuchezesha bahati nasibu ya Sh. 967,630,639.93 mali ya TRA.

Ilidaiwa kuwa kati ya Agosti, mwaka jana na Mei 23, mwaka huu, jijini Dar es Salaam, kwa makusudi aliisababishia TRA hasara ya kiasi hicho cha fedha kwa kukwepa kulipa kodi ya mashine hizo.

Pia ilidaiwa katika shtaka lingine kuwa katika tarehe hizo, mshtakiwa huyo kwa makusudi alitakatisha Sh. 967,630,639.93 wakati akijua zilitokana na makosa ya udanganyifu.

Mshtakiwa huyo hakutakiwa kujibu chochote kwa kuwa kesi inayomkabili ni ya uhujumu uchumi na mahakama hiyo haina mamlaka ya kuisikiliza. Jamhuri ilidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika.

Hakimu alisema mshtakiwa apelekwe mahabusu mpaka Julai 10, mwaka huu kesi hiyo itakapotajwa.



Wafanyabiashara wadogo maarufu kama machinga wakiwa wamepanga bidhaa zao kwenye eneo la upanuzi wa barabara ya Bagamoyo, eneo la Mwenge, jijini Dar es Salaam jana, licha ya kuondolea katika eneo hilo. **PICHA: ATLEY TIMOTHY- TUDARCO**

# Waliovunjiwa nyumba waomba huruma ya JPM

**Na Mwandishi Wetu,** BAGAMOYO

ZAIDI ya wakazi 600 wa vitongoji vya Changwahela na Kiharaka katika Kata ya Mapinga wilayani hapa, wamemwomba Rais John Magufuli kuwasaidia kupata haki ya maeneo yao baada ya kuvunjiwa nyumba zao na polisi wakidaiwa kuwa ni wavamizi.

Wakizungumza na Nipashe juzi wakiwa katika maeneo yao walikovunjiwa nyumba zao, wananchi hao walisema kwa sasa wanaishi kama wakimbizi wakati ni Watanzania halali.

Mmoja ya wananchi hao, Ester Samwel, akizungumza kwa uchungu, alisema wamenyanyaswa na askari polisi kwa muda mrefu na kwamba walikuwa wakifika katika maeneo yao wanapiga milango mateke na wakishaingia ndani wanawatoa nje na kisha kuanza kuchoma moto nguo zao.

Samwel alisema mbali na kuchomewa nguo zao lakini pia wamekuwa wakipigwa mabomu ya machozi bila sababu za msingi, huku wakilazimishwa kuondokana katika maeneo hayo.

"Tunajua Rais wetu ni wa wananchi wote hasa wanyonge, tunamwomba atusaidie maana tunanyanyasika sana katika nchi yetu kwa sababu ya watu wenye pesa.

Kama unavyoona tumevunjiwa nyumba zetu na sasa tunalala nje na watoto wetu wachanga huku tukiwa hatujui hatima yetu," alisema Samwel.

Naye Emmanuel Mgeni alisema wameishi katika maeneo hayo kwa zaidi ya miaka 10, lakini hivi karibuni waliletewa samansi kutoka Mahakama ya Ardhi na Nyumba Kibaha ikiwataka kufika mahakamani hapo kwa ajili ya shauri la madai linalohusu maeneo wanayoishi.

Mgeni alisema cha kushangaza wakati shauri hilo likiwa linaendelea na hukumu ikiwa haijatolewa, polisi wamekuwa wakifika katika maeneo yao mara kwa mara na kuwabughudhi na sasa wameamua kuwavunjia nyumba na kuwaacha wakiwa hawana mahali pa kulala.

"Tunamwomba Rais wetu pamoja na vyombo vinavyohusika waingilie kati watusaidie maana ni heri hukumu ingekuwa imetoka tukajua tumeshindwa hapo tusingekuwa na la kusema. Lakini pia utaratibu wa kuvunjiwa kwa kibali cha mahakama si huu ambao unafanywa kwetu na askari polisi," alisema Mgeni.

Paulo Mbegezi, mmoja wa waathirika hao, alisema kwa sasa hata watoto wao hawaendi shuleni kutokana na nguo kuchomwa moto.

Mbegezi alisema ni vyema vyombo vinavyohusika vikaingilia kati mapema vinginevyo watawaondoa wakiwa wamefikwa na umauti kwa kuwa hawako tayari kuondoka na kupoteza haki yao.

"Kama kweli kuna mtu anasema maeneo hayo ni ya kwake, ni vyema angesubiri uamuzi wa mahakama lakini si kama hivi tunavyonyanyaswa utafikiri sisi ni wakimbizi ndani ya nchi yetu," alisema Mbegezi.

## Waomba ofisi ya TRA Kaliua

**Na Tiganya Vincent,** KALIUA

BAADHI ya wafanyabiashara wilayani Kaliua, wameiomba Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuwajengea ofisi kwenye wilaya yao ili kuwapunguzia gharama za kusafiri umbali mrefu kwenda Urambo ili kupata huduma.

Wafanyabiashara hao walitoa kilio hicho juzi wakati wa semina ya uelimishaji kuhusu ulipaji kodi.

Walisema ukosefu wa ofisi katika wilaya hiyo, umewasababisha kuchelewa kukamilisha taratibu za ulipaji wa kodi mbalimbali, hivyo kujikuta wakilipa faini ambazo wasingepaswa kulipa kama ofisi ingekuwa katika wilaya yao.

Mtatilo Mwita, ambaye ni mfanyabiashara wa bidhaa mbalimbali, alisema kwa kufuata ofisi ya TRA Urambo kwa ajili ya kukamilisha taratibu za malipo kodi ambazo wanapaswa kulipa, umesababisha wakati mwingine kulipa adhabu kwa sababu ya kuchelewa kukamilisha malipo hayo.

Alisema umbali wa ofisi ya TRA kutoka eneo wanalofanyia biashara, umesababisha wafanyabiashara wengi kuchelewa kukamilisha taratibu pindi wanapokutana na tatizo la mfumo wa malipo kutofanya kazi.

Naye Mwandu Manoni aliomba TRA kusogeza huduma karibu na wafanyabiashara ili kujenga mazingira rafiki ya ulipaji kodi kwa ajili ya kuepuka ukwepaji unaotokana na mazingira magumu ya kukamilisha taratibu za malipo.

Wakati huo huo, baadhi ya wafanyabiashara wa Halmashauri ya Wilaya ya Nzega na Sikonge wameomba TRA kuongeza watumishi ili kuwarahisishia ulipaji kodi.

Walisema uchache wa watumishi wa TRA kumesababisha kulipa adhabu kwa sababu ya kuchelewa kulipa kodi.

Mfanyabiashara Juma Shamba alisema uchache wa watumishi umesababisha kutopata huduma kwa wakati na kujikuta wakiingia katika mtego wa kufanya makosa.

Akijibu hoja za wafanyabiashara, Meneja wa TRA Mkoa wa Tabora, Thomas Masese, alisema wanatarajia kupata watumishi wapya na pindi watakapowapata baadhi yao watawagawanya katika maeneo yenye upungufu ikiwamo Nzega.

## HABARI KITAIFA



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (kushoto), akiangalia kipeperushi cha Benki ya NMB, alipotembelea banda la benki hiyo kwenye maonyesho ya Kongamano la Uwekezaji Mkoa wa Dodoma juzi. **PICHA: NMB**

# TOL yatoa gawio wanahisa bil. 1/-

**Na Mwandishi Wetu,**

KAMPUNI ya TOL Gases Limited, imetangaza kutoa gawio la Sh. bilioni moja kwa wanahisa wake ikiwa ni mara ya kwanza kufanya hivyo kwa kipindi cha miaka 20 tangu ilipoingia katika Soko la Hisa Dar es Salaam(DSE). Hayo yamesemwa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo inayotengeneza gesi za viwandani na hospitalini, Daniel Warungu, wakati wa Mkutano wa Wanahisa kwa mwaka 2018 uliofanyika jijini Dar es Salaam.

Alisema kutokana na mageuzi makubwa ya kiutendaji ambayo yamefanyika katika menejimenti, kwa sasa wamekuwa wakijiendesha kwa faida na kwa mwaka wa fedha wa 2018, wamepata faida ambayo imewezesha kuanza kutoa gawio ikiwa mara ya kwanza kufanya hivyo tangu mwaka 1998. "Kwa kweli hivi sasa tunajivunia kwani tunajiendesha kwa faida ndiyo maana leo (jana) tumekutana na wanahisa kutangaza kugawa gawio ambapo hisa moja ni Sh. 17.37. Jumla ya gawio ambalo limetengwa kwa wanahisa ni Sh. bilioni moja.

"Tunawashukuru wanahisa wote, menejimenti na Bodi ya Wakurugenzi kwa namna ambavyo wameshirikiana kuhakikisha kampuni yetu inafanya vizuri kuuza bidhaa zetu katika soko," alisema Warungu.

Alisema katika kuhakikisha wanapata faida, waliamua kupunguza matumizi yasiyo ya lazima na kuongeza uzalishaji wa bidhaa zenye ubora na matokeo yake wanajipongeza kwa mafanikio yanayokwenda sambamba na utoaji wa hisa kwa wanahisa wote. Kuhusu mikakati yao, alisema wanatarajia kununua mitambo miwili na kuongeza magari kwa ajili ya kusafirisha bidhaa katika nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Afrika Mashariki. Alifafanua kuwa uamuzi wa Serikali ya Awamu ya Tano kuhamasisha ujenzi wa viwanda umeisaidia kampuni yao kuongeza idadi ya wateja.

"Tunalo soko la uhakika ndani ya nchi ya Tanzania, lakini pia tunafanya biashara zaidi ya kuuza bidhaa zetu kwenye nchi mbalimbali za Afrika. Katika kufurahia mafanikio yetu, tunakwenda pamoja na kuweka mikakati ya kujiimarisha zaidi," alisema Warungu.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya TOL Gases Limited, Michael Shirima, aliwahakikishia wanahisa wote kuwa wamejiridhisha na utendaji kazi wa menejimenti ya sasa ambayo inafanya kazi vizuri na wameanza kuona matumaini makubwa ya kufanya vizuri.

"Tunawapongeza menejimenti yetu, huko nyuma kwa miaka mingi hatukuwa tunafanya vizuri na ndio maana hatujapata gawio lakini safari hii tunapata gawio. Hata hivyo menejimenti tuliiuliza zaidi ya mara moja hili la gawio litakuwa kila mwaka au itakuaje. Wametujibu kuanzia sasa itakuwa ni kila mwaka kwani wanakwenda vizuri," alisema.

# Afariki dunia akizuia lori kwa gogo

**Na Said Hamdani, LINDI**

MKAZI wa Mtwara, Azizi Natende (33), amefariki dunia kwa kukanyagwa na lori alilokuwa anajaribu kulizuia kwa gogo baada ya kushindwa kupanda Mlima Kinyope ulioko Kata ya Rutamba wilayani mkoani Lindi.

Taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, Pudensiana Protasi, ilieleza kuwa ajali hiyo ilitokea juzi saa 12 asubuhi.

Alidai lori hilo aina ya Nissan lenye namba za usajili T 670 ABU, lilikuwa linaendeshwa na Juma Natindi (52), mkazi wa Mtwara Mjini.

Katika taarifa hiyo, ilidaiwa kuwa lilipokuwa linapandisha mlima huo, lori hilo lilishindwa na kurudi nyuma, kitendo kilichosababisha utingo huyo ateremke kuweka kigogo kwa lengo la kuizuia.

"Yule utingo baada ya kuona gari lao linashindwa kumalizia ule Mlima Kinyope, aliteremka kwa lengo la kuweka gogo, lakini akafeli na kukanyagwa na kukatisha uhai wake," ilidaiwa katika taarifa hiyo.

Alisema mwili wa marehemu baada ya kufanyiwa uchunguzi na wataalamu wa Hospitali ya Sokoine mkoani Lindi, ulikabidhiwa kwa ndugu na jamaa kwa ajili ya kuuzika.

# Migogoro ndoa yachangia ukatili kwa watoto

**Na Mwandishi Wetu**

ONGEZEKO la migogoro ya ndoa, limetajwa kuwa chanzo kikubwa cha vitendo vya ukatili nchini pia kusababisha watoto kukosa malezi ya wazazi wote wawili.

Hayo yalibainishwa jana jijini Dar es Salaam katika kikao kati ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na wahariri wa vyombo vya habari katika kujengewa uelewa kuhusu Ajenda ya Kitaifa ya Wajibu wa Wazazi /Walezi wa Malezi na Matunzo ya Familia.

Kwa mujibu wa takwimu za Ofisi ya Ustawi wa Jamii, katika miezi tisa kuanzia Julai, mwaka jana hadi Machi, mwaka huu, mashauri ya ndoa 16,832 yalipokewa ukilinganisha na 13,382 kwa mwaka 2017/2018.

Akizungumza kwa niaba ya Katibu Mkuu Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. John Jingu, Kamishna wa Ustawi wa Jamii, Dk. Naftali Ng'ondi, alisema vyombo vya habari ni wadau muhimu katika kutoa elimu kwa jamii, hivyo vina wajibu kuhakikisha vinatoa elimu kusaidia ujenzi wa malezi bora kwa familia na watoto nchini.

Dk. Ng'ondi alisema vitendo vya ukatili vimezidi kukithiri nchini, hivyo vyombo vya habari nchini vina wajibu wa kuendeleza ajenda hiyo ili kusaidiana na serikali katika kupambana navyo.

Alisema kwa mujibu wa utafiti wa hali ya ukatili dhidi ya watoto uliofanywa na wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kuhudumia Watoto la Unmoja wa Mataifa (Unicef) wa mwaka 2011, mtoto mmoja kati ya watatu wa kike na mmoja kati ya saba wa kiume walifanyiwa vitendo vya ukatili kabla ya kufikisha umri wa miaka 18.

Dk. Ng'ondi alisema asilimia 72 ya wasichana na 71 ya wavulana walifanyiwa ukatili wa kimwili na pia robo ya watoto walifanyiwa ukatili wa kiakili.

Naye Kaimu Mkurugenzi Idara ya Maendeleo ya Mtoto kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mwajuma Magwiza, alisema wadau wote wakiwamo wahariri na waandishi wa habari, wana wajibu wa kuhakikisha watoto wanapata malezi na makuzi bora kwa kuhakikisha wanajenga maadili na kuimarisha mila na desturi katika kujenga jamii iliyo bora.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Siasa ziepukwe sasa kuijenga Taifa Stars

**TIMU** ya Taifa ya Soka ya Tanzania, 'Taifa Stars' imeendelea kufanya vibaya kwenye michuano ya Mataifa ya Afrika (Afcon) 2019 nchini Misri, baada ya juzi kupoteza mechi yake ya pili mfululizo kwenye hatua ya makundi.

Stars ambayo ipo Kundi C pamoja na Algeria, Senegal na majirazao, Kenya, hii ni mara ya kwanza kushiriki michuano hiyo ya Afcon katika kipindi cha miaka 39, ikiwa ni tangu iliposhiriki fainali za Nigeria mwaka 1980.

Katika mechi yake ya kwanza kwenye michuano hiyo, Taifa Stars ilikubali kipigo cha mabao 2-0 dhidi ya Senegal kabla ya juzi kuchapwa 3-2 dhidi ya Kenya ('Harambee Stars), mato hayo yanaifanya Stars kuburuza mkia katika kundi lake, hivyo sasa inasubiri tu kukamilisha ratiba kwa kucheza dhidi ya Algeria Julai Mosi. Hata hivyo, mbali na maandalizi ya Stars ambayo hayakuwa ya kuvutia lakini kumekuwapo na mihemko mikubwa kutoka makundi mbalimbali husUsan ya kisiasa zaidi, ambayo kila moja limekuwa na hoja zake kuhusu timu hiyo baada ya kupoteza mechi zake za awali.

Kwa ujumla maoni yanayotolewa huku kila moja likivutia upande wake, yamekuwa si ya kujenga kwa wakati huu ambao wachezaji wa Taifa Stars walikuwa wanapaswa kujengwa kisaikolojia zaidi kuliko tuhuma mbalimbali ambazo zimekuwa zikielekezwa kwao pamoja na benchi zima la ufundi.

Maoni mbalimbali yalianza kutolewa kutoka kwa wabunge, na wengi wakionyesha wazi kutomkubali Kocha Mkuu wa Stars, Mnigeria Emmanuel Amunike na wengine wakionyesha kutoridhishwa na kikosi anachokipanga, hayakuwa ya kujenga timu hiyo kwani yalitolewa mara tu baada ya kupoteza mchezo wake wa kwanza dhidi ya Senegal wakati wakihitaji faraja kipindi hicho. Aidha, wapo baadhi ya viongozi walioonyesha kuvutia upande wao zaidi kwa kuwatia moyo wachezaji huku wakiamini hamasa yao inaweza kuleta ushindi kwa Stars kuelekea mchezo wake wa pili dhidi ya Kenya.

Ni kweli kabisa Stars ilihitaji hamasa ya aina hiyo kwa kuungwa mkono kwa kila hatua hata pale ilipoonekana kufanya vibaya, lakini kama Watanzania, haikustahili kuanza kugawanyika makundi mawili na kila moja kuvutia upande wake wakati huu 'askari wetu hao wakiwa vitani'.


Sisi Nipashe daima tunaamini umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu, hivyo moja kwa moja waliozidi kuitia udhaifu Stars ni Watanzania wenyewe hususan baadhi ya wabunge na wadau wengine wa soka walioanza kumkosoa hadharani kocha pamoja na baadhi ya wachezaji wake. Wenzetu Kenya, walitumia wachezaji wa zamani wa timu hiyo ya taifa akiwamo McDonald Mariga kwenda kuwahamasisha Harambee Stars, lakini Tanzania imekuwa ikitanguliza siasa mbele hata pale ambapo wanasiasa walipaswa kubaki kama washangiliaji na wawezeshaji kifedha tu kwa timu hiyo. Tunaamini mchezaji mkongwe anapopewa fursa ya kwenda kuwahamasisha wachezaji, kuna kitu kikubwa wanaweza kujifunza kutoka kwake kuliko namna ambavyo wanasiasa na viongozi mbalimbali wa serikali wamekuwa mstari wa mbele zaidi kwenda moja kwa moja kuzungumza na wachezaji.

Hatulipingi hilo, lakini linapaswa kufanyika kwa umoja na ushirikiano mkubwa kuliko kama inavyoendelea katika timu ya taifa na kila mmoja akitaka kuitumia kama daraja la kujipatia umaarufu wakati Watanzania wanataka mafanikio kisoka. Tunaona ipo haja sasa wanasiasa na viongozi wengine wa serikali kuacha kuitumia Stars kama daraja lao la kujipatia umaarufu kisiasa kwa kuwa tunafahamu fika wengi hutumia mlango wa soka kujipatia wafuasi wengi kutoka katika mchezo huo unaoongoza kwa kuwa na mashabiki wengi duniani. Tayari Stars, imepoteza nafasi Afcon, hivyo makundi ya kisiasa yaliyojitokeza ni vema sasa kumulika na kutoa michango yao hususan ya kifedha ili kuijenga kuelekea michuano ijayo badala ya kuanza kuvutana na kutafuta mchawi aliyechangia kushindwa kupata mafanikio nchini Misri.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Watanzania tusilalamike, tuna cha kujifunza Afcon

Na Adam Fungamwango

**BAO** la dakika ya 80 lililofungwa na Michael Olunga liliwanyong'onyesha Watanzania wote waliokuwa wakifuatilia mechi ya fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2019 zinazoendelea kunguruma nchini Misri.

Olunga huyu huyu ambaye misimu mitatu iliyopita alikuwa akigombewa na Klabu za Simba na Azam, lakini Gor Mahia ikamuuza Ulaya, ndiye alikuwa mwiba kwenye safu ya ulinzi ya Taifa Stars.

Kilichowaumiza zaidi Watanzania ni kwamba hadi mapumziko Stars ilikuwa inaongoza kwa mabao 2-1 na kwa jinsi soka lilivyokuwa likitandazwa, ilitegemewa kutoka na ushindi kwenye mechi hiyo.

Ushindi ulikuwa bayana kwa sababu Harambee Stars, timu ya Taifa ya Kenya, haikuwa ya kutisha sana kama ilivyokuwa kwa Senegal. Hawa ni majirani, lakini pia aina ya soka linafanana.

Hiyo yote haikuwa dawa, mwisho wa siku, Stars ilikubali kichapo cha mabao 3-2, na kuwa ni kipigo cha pili kutoka kile cha kwanza cha mabao 2-0 dhidi ya Senegal.

Kumekuwa na maneno mbalimbali kama kawaida ya Watanzania kutoka huku na kule, kila mmoja akieleza kwa namna yake sababu za kufungwa. Lawama kama kawaida hazikosekani.

Pamoja na yote haya yanayotokea nchini Misri, Watanzania wanapaswa kujua kuwa Taifa Stars inacheza michuano hiyo kwa mara ya kwanza baada ya miaka 39.

Mara ya mwisho ilikuwa ni 1980, fainali zilizofanyika nchini Nigeria, baada ya kufuzu mwaka 1979, miaka 40 iliyopita.

Hii inaonyesha kuwa Stars ilikuwa bado changa kwenye michuano hiyo kuweza kufanya vizuri.

Kuna nchi ambazo ni kawaida yao kutinga hatua za fainali, lakini zina miaka kibao hazijachukua ubingwa na badala yake zinatolewa mapema tu kwenye michuano hiyo, sembuse Tanzania ambayo imetinga baada ya miaka mingi kupita?

Kucheza tu hatua hii kwa Taifa Stars inapaswa kupongezwa na wala si kubezwa na kinachotakiwa hapa ni kuchukulia kama changamoto kwa kile kilichotokea.

Kwa serikali na Shirikisho la Soka nchini (TFF), wanapaswa kujifunza kwanza kuwa soka kwa sasa ni kazi kama kazi zingine na si burudani baada ya kazi. Na wala hakuna siasa katika hili.

Wachezaji wetu wanapaswa watengenezewe mazingira ya kutoka kwenda kucheza nje ya nchi na si kuweka kanuni za kuwazuia wageni ili kupata Stars inayotokana na klabu za Simba, Yanga na Azam.

Ukiangalia hata wachezaji wa Stars wanaocheza nje ya nchi wanaonekana kuwa wako vizuri kuliko wachezaji wanaocheza ligi ya ndani. Ukimwangalia Mbwana Samatta, Thomas Ulimwengu, Simon Msuva na sasa Farid Mussa, wanaonekana kabisa kuna vitu adimu kabisa tofauti na wenzao.

Hata Kenya ambao ni majirani zetu wana idadi kubwa ya wachezaji wanaocheza soka la kulipwa nje ya nchi kuliko Tanzania.

Badala ya kulalamikia kwa nini tumefungwa, nani kasababisha timu ifungwe, inapaswa kuandaa michuano mingi ya vijana, na wale watakaoonekana wana vipaji, basi serikali na TFF ibebe jukumu la kuwaombea kwenda kwenye academy za nchi marafiki kwa ajili ya kutunzwa, kufunzwa soka na kusomeshwa ili waweze kuikomboa nchi miaka ya mbele na si wachezaji kubaki hapa hapa na kukaa mitaani, kitu ambacho kinasababisha viwango vyao kushuka na maisha yakishakua magumu wanaacha soka na kufanya shughuli zingine za kujikimu kimaisha.

Ukiziangalia timu nyingi zenye wachezaji wanaocheza nje ya nchi, kama vile Senegal, Nigeria, Cameroon, pamoja na kwamba wana miili mikubwa na nguvu, si kwamba wana vipaji sana, ila wana misingi mizuri ya kukuzwa kisoka na wanatumia miili na akili zao vizuri zaidi kuliko wachezaji ambao wanatoka tu mitaani. Tunaondoka Afcon, lakini tuondoke na kitu tulichojifunza.

# Wateja wa Vodacom M-Pawa waongezeka

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Biashara Afrika (CBA) na kampuni ya simu za mikononi ya Vodacom, zimetangaza washindi wa droo ya tatu kwa ajili ya promosheni ya kuadhimisha miaka mitano ya huduma ya M-Pawa yenye lengo la kuwahusisha kifedha wateja wake kwa kuwazawadia.

Promosheni hiyo ilifanyika katika makao makuu ya benki hiyo, jijini Dar es Salaam.

Akizungumza katika droo hiyo iliyofanyika jana, mwakilishi wa CBA, Maria Marbella, alisema kwa sasa watumiaji wa M-Pawa wameongezeka kwa kasi na kufikia milioni 8.5 tangu izinduliwe, huku wateja hao wengi wakiwa ni wanawake ambao ni wafanyabiashara, vijana na watu wanaoishi maeneo ya vijijini ambako huduma za kifedha na benki ni za kiwango kidogo.

"Kampeni hii ya miaka mitano ya M-Pawa imelenga kudumu kwa wiki sita na leo (jana) ikiwa ni droo ya sita na zaidi ya washindi 1,000 wamepatikana mpaka sasa, baadhi ya washindi wameondoka na mara mbili ya akiba ya kuanzia Sh. 1,000 mpaka Sh. 200,000 za Kitanzania, simu za kisasa, vocha na zawadi zingine huku washindi wengine wakiongezeka kwenye droo zilizobaki," alisema.

"Mshindi wa kwanza wa promosheni hii atazawadiwa Sh. milioni 15 kwenye droo ya mwisho, hivyo tunaendelea kuwasisitiza watumiaji wa M-Pawa kuweka akiba na kurejesha mikopo mapema ili waweze kupata nafasi ya kushinda," aliongeza.

Aliongeza kuwa M-pawa ni huduma iliyoleta mapinduzi ya kibenki ambayo inaruhusu watumiaji kuweka akiba kwa njia ya simu, na kupata faida kutoka kwenye akiba yao na hatimaye kuongeza kiwango cha mikopo yao.

"Kutumia njia hii tunawawezesha wateja wetu kuendeleza mitaji yao kwa ajili ya baadaye na kufikia baadhi ya ndoto zao. Tunawapongeza washindi watatu wa droo pamoja na washindi wetu wote waliopita. Hii inatupa faraja kubwa kuwazawadia wateja wetu waaminifu na tunafurahia kuona wananufaika kutokana na huduma zetu," alisema Marbella.

Alifafanua kuwa ili kushiriki na kushinda kwenye droo hiyo, mteja wa M-Pawa anatakiwa kuweka akiba isiyopungua Sh. 1,000, kukopa na kurudisha mapema mkopo wake na hapo papo atakuwa ameingia kwenye droo na kujiwekea nafasi ya kushinda.

Baadhi ya washindi wa droo za M-Pawa tatu zilizopita ni Mangu Zanura, Nyerenga Rahim, Robert Tuisenge, Mwafumba Martha, Ayilla Agness, Kayombo Hilda, Mollel Charity, Gwandu Elizabeth, Agust Emannuel, Tezeyo Abinal, Mwita Joseph, Haule Reginberti na Kabona Fadhili.

# Serikali kulinda maslahi ya waajiri, waajiriwa

**Na Beatrice Shayo**

SERIKALI imesema lengo la kuweka mazingira rafiki katika uwekezaji ni kulinda maslahi ya waajiri na waajiriwa.

Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera na Uwekezaji, Dorothy Mwaluko, alisema hayo wakati wa mkutano wa 60 wa mwaka wa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE).

Alisema lengo lingine ni kuziba pengo la ujuzi na wahitaji sokoni na wahitimu waliopo pamoja na watakaoongezeka.

Alisema mwaka 2014 kupitia maabara ya kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini, iliazimia kuongeza kiwango cha nguvu kazi chenye ujuzi na walijulishwa ni asilimia 17 ya waajiri wenye viwango stahiki.

Alisema mwaka jana waliazimia kiwango hicho kuongezeka hadi kufikia asilimia 46, hivyo wanasubiri ifanyike tathmini hasa kwa wanaohusika na masuala ya kazi na ajira ili waone kama wametimiza azma ya asilimia 46.

Alisema katika kutekeleza azima hiyo, serikali imeendelea kuwa na mikakati mbalimbali ya kuongeza ujuzi wa nguvu husasani vijana.

"Kwa kutambua hilo serikali imeipa jukumu sekta binafsi la kusimamia mabaraza ya ujuzi ambayo yamezinduliwa hivi karibuni yanalenga kuboresha ujuzi na stadi za kazi miongoni mwa nguvu kazi iliopo hapa nchini," alisema.

Aidha, alisema ATE itakuwa mstari wa mbele katika utekelezaji wa kukuza stadi za kazi na ujuzi za nguvu kazi zilizopo nchini.

Alisema chama cha ATE kinatakiwa kuunga mkono jitihada zinazofanywa na rais katika maendeleo anayoyafanya.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa ATE, Aggrey Mlimuka, alisema huo ni mkutano mkuu wa mwaka na mada ni kutumia uwezo wa Watanzania katika kuhamasisha uwekezaji na kazi za siku zijazo.

Alisema kama chama cha waajiri mwaka huu ni mzuri kwao kwa sababu Shirika la Kazi Duniani (ILO) ambalo hufanya nao kazi kwa ukaribu wametimiza miaka 100 na wamewapa malengo wanayotakiwa kuyafanya.

"Shirika hili wanataka kuangalia miaka 100 ijayo masuala ya kazi yatakuwa ya aina gani, lakini tunahusisha na yale yanayotokea nchini kwetu kuhusiana na uwekezaji," alisema.

Dk. Mlimuka alisema changamoto ni ujinga, maradhi na umaskini bado unaendelea kuwaathiri wananchi.

Alisema utafiti bado unaonyesha ujuzi wa watu bado upo chini na ni changamoto inayotakiwa kufanyiwa kazi, ndiyo maana wamewataka waajiri ambao vijana kuwasomesha.

Alisema uchumi wa kati wa viwanda unataka nguvu kazi ya watu wenye elimu ya kutosha kuendana na changamoto za uchumi.



Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad (kulia), akiteta jambo na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Nangenjwa Kaboyoka, kabla ya uzinduzi wa ripoti ya uwajibikaji ya mwaka 2017/18, iliyoandaliwa na Taasisi ya Wajibu, mjini Moshi, mkoani Kilimanjaro jana. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Vyeti vya kuzaliwa kutolewa Sabasaba

**Na Salome Kitomari**

WAKALA wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA), unatarajia kusajili, kutoa vyeti vya kuzaliwa na ushauri wa kisheria kwa wananchi watakaotembelea banda lao katika viwanja vya Sabasaba jijini Dar es Salaam.

Ushauri huo utakuwa kwa wanaotaka kuandika wosia na mirathi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa juzi na Meneja Masoko na Mawasiliano wa Rita, Josephat Kimaro, wananchi watakaojiandikisha watapatiwa vyeti vya kuzaliwa papo hapo.

Alisema huduma zingine zitakazotolewa ni elimu kwa umma kuhusu huduma za Rita, kupokea maoni, maswali na ushauri.

"Mwaka jana tulitoa huduma kwa zaidi ya wananchi 5,520 walisajiliwa na kupata vyeti vya kuzaliwa, mwaka huu tumeongeza watumishi watakaotoa huduma," alisema.

Kimaro alisema kwa mwaka huu wamejiwekea lengo la kusajili zaidi ya wananchi 1,000.

"Ili kusajiliwa na kupata cheti cha kuzaliwa mwananchi anatakiwa awe amezaliwa katika mkoa wowote Tanzania Bara na awe na viambatisho muhimu," alisema.

Alivitaja viambatisho hivyo kuwa ni cheti cha ubatizo, cheti cha falaki cha mwombaji, cheti cha kumaliza elimu ya msingi au sekondari, pasi ya kusafiria.

HABARI KITAIFA

# Watanzania 9 wauawa Msumbiji

**Na Romana Mallya**

WATANZANIA tisa wameuawa kwa kupigwa risasi na wengine sita kujeruhiwa Msumbiji baada ya kuvamiwa wakiwa kwenye mashamba yao ya mpunga na watu wanaodaiwa kuvaa sare zinazofanana na za jeshi la nchi hiyo.

Akiwa Mtwara jana, Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP), Simon Sirro, (pichani) aliiambia Nipashe kuwa juhudi za kuwasaka waliofanya mauaji hayo zinaendelea.

Alisema tukio lililotokea katika Kijiji cha Nkole kilichoko upande wa Msumbiji, eneo ambalo ni mpakani mwa Tanzania na nchi hiyo.

Alibainisha kuwa katika tukio hilo, watu 11 waliuawa, wawili wakiwa ni raia wa Msumbiji.

"Ninawaambia wauaji kuwa damu ya Watanzania haiendi bure, walioua tutawasaka kwa kushirikiana na majeshi ya Msumbiji kuhakikisha tunawakamata wakiwa hai ama wamekufa. Wahalifu hawa baada ya kufanya vurugu waliondoka na wanawake wawili wa Tanzania na mtoto mmoja ambao hadi sasa (jana jioni) hawajapatikana," alisema.

"Hawa Watanzania walikuwa Msumbiji wakijishughulisha na shughuli za kilimo cha mpunga, wakiwa kwenye mashamba yao ambako wameweka vibanda vya muda, ghafla walivamiwa na watu wakiwa wamevalia sare zinazofanana na za Jeshi la Msumbiji na kuwaua baadhi na wengine kuwajeruhi.

"Tumewatembelea majeruhi, wapo Watanzania sita na wengine wawili ni raia ya Msumbiji wanaendelea na matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Ligula," alisema.

IGP Sirro alisema Jeshi la Polisi linaendelea na operesheni za nguvu ili kuwasaka wale wote waliohusika na kuhakikisha watu hao hawavuki mipaka kuingia Tanzania.

"Tunatoa tahadhari kwa wananchi kuwa Msumbiji siyo salama, kipo kikundi kinachochoma nyumba na kuua watu," alisema.



# Waziri atangaza kuifumua TBA

INATOKA UK. 3

walioko kwenye mradi huo na kutafuta msimamizi wa mradi wa TBA ambaye kitaaluma ni mhandisi ili ausimamie.

"Baada ya kuzungumza na hawa niliowakuta hapa, nimebaini wameingiliana katika majukumu ya utendaji kazi, mimi ni mhandisi wa barabara, siwezi kwenda kufanya miradi ya maji, hatuendi hivyo," alisema.

Waziri huyo alimwagiza Katibu Mkuu - Sekta wa Ujenzi ampelekee majina ya wakala wasimamizi wa miradi inayosimamiwa na TBA nchini ili kuona taaluma zao.

"Ninataka kuwe na watu wenye taaluma zinazotakiwa kwa sababu hatuwezi kuzifanyia mafunzo fedha za serikali maana tunaleta watu wenye taaluma nyingine kwenye miradi ili wafanye mafunzo. Hatuwezi kufika, naona mpango sio mzuri.

"Ninataka miradi yote nchi nzima wale wakala wasimamizi wa miradi nipate majina yao kwa sababu nilikwenda Songwe nikakuta mhandisi mmoja anasimamia miradi kwenye halmashauri zote, hili haliwezekani, mradi ni kama mtoto mchanga, mama mmoja hawezi kusimamia watoto wachanga sita.

"Kila jengo, kila mradi kunatakiwa kuwe na wakala msimamizi wa kudumu, ninataka miradi yote ya TBA nipate majina ya wasimamizi wakuu wa miradi hiyo na mapendekezo yangu ni kuweka watu wenye taaluma za uhandisi wa ujenzi, taaluma nyingine ziwepo, lakini mtu huyu lazima awapo pia," alisema.

Awali, Kaimu Mkurugenzi Idara ya Ushauri TBA, Kileo Khamis, ambaye ni kitaaluma ni mbunifu majengo, alimweleza waziri huyo kuwa Oktoba mwaka 2016, ujenzi huo ulianza rasmi.

Alibainisha kuwa usanifu uliotengenezwa ni kwamba jengo moja litakuwa na maghorofa matano na kila ghorofa kuwa na uwezo wa kuchukua kaya 16.

# Tundu Lissu apoteza ubunge

INATOKA UK. 3

fulani, naendelea na jambo fulani hivi, hakuna chochote, yaani Spika kama hayupo vile, hilo la kwanza.

"Lakini la pili, waheshimiwa wabunge tunatakiwa sote tujaze taarifa kila mwaka mara moja zenye maelezo ya mali na madeni kama katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inavyotaka na utaratibu unataka ujaze nakala mbili na nakala zote uzipeleke Ofisi ya Spika, halafu Ofisi ya Spika ndiyo inapeleka nakala moja kule maadili na kubakia na nakala moja.

"Lakini huwa tunaipata ile nakala na kupeleka zote mbili tunaiweka kwa ajili ya kumbukumbu zetu hapa bungeni, ndiyo matakwa yenyewe.

"Baada ya kuona kwenye kumbukumbu zangu hakuna nakala yoyote ya fomu za maadili za Mheshimiwa Tundu Lissu (pichani), nilichukua jukumu la kupata uhakika wa jambo hili kwa Kamishna wa Maadili na nilijibiwa kwa barua kwamba Lissu hajawasilisha taarifa yoyote kuhusiana na fomu zake ziko wapi."

**CHADEMA WAJIPANGA**

Muda mfupi baada ya Spika kutangaza uamuzi huo, Ofisa Habari wa Chadema, Tumaini Makene, alisema chama chao kimemsikia kiongozi huyo wa Bunge akitangaza jambo hilo zito na kinajipanga kutoa kauli.

Lissu (51), ambaye pia Mwanasheria Mkuu wa Chadema, alishambuliwa kwa kupigwa risasi na watu wasiojulikana Septemba 7, 2017.

Wakati anafanyiwa unyama huo, mtaalamu huyo wa sheria alikuwa anajiandaa kushuka kutoka kwenye gari lake nyumbani kwake Area D mjini Dodoma, ikiwa ni muda mfupi baada ya kuahirishwa kwa kikao cha mchana cha Bunge ambacho pia alipata nafasi ya kuchangia hoja.

Baada ya shambulio hilo, Lissu alipelekwa kwenye Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma na kupatiwa matibabu ya awali kisha kusafirishwa kwenda Kenya kwa matibabu ya kibingwa.

Mbunge huyo aliondoka Kenya kwenda Ubelgiji akipita Amstedam, Uholanzi Januari 6, mwaka jana.

Imekuwa ikielezwa na baadhi ya wachambuzi wa masuala ya siasa nchini kuwa kuna uwezekano mkubwa Lissu akapeperusha bendera ya Chadema kuwania kiti cha urais wa Tanzania katika Uchaguzi Mkuu wa mwakani.

Hivi karibuni, Lissu alitoka hospitalini Ubelgiji na kufanya ziara katika baadhi ya nchi za Ulaya na Amerika na kuweka wazi kuwa kama chama chake kitaona anafaa kukiwakilisha kuwania kiti cha Rais wa Tanzania mwakani, atakuwa tayari kufanya hivyo.



# CAG afunguka kodi kwa mtutu

INATOKA UK. 2

kubwa sana, vitabu vitatu, vinne na Watanzania si wasomaji wa vitabu vikubwa. Kwa hiyo, sisi tunachofanya, ripoti yenye kurasa 300 au 400, tumetengeneza ndogo ya kurasa 20 au 22 ambapo mambo gani CAG ameibua ambayo yana umuhimu mkubwa zaidi kwa wananchi wa Tanzania.

"Ndiyo hayo tunayaangalia, tunayachambua, katika kuyachambua tunaeleza madhara haya yaliyoibuliwa kutotekelezwa na vilevile tunasaidia watekelezaji waliopendekezwa na CAG kwamba ni nini kifanyike ili mapendekezo hayo ya CAG yafanyiwe kazi."

"Ripoti hizi zimeshazinduliwa na tutakuwa na mada inayozungumzia uboreshaji wa makusanyo ya mapato ya serikali hasa mapato yanayotokana na kodi.

"Kama tunavyojua mahitaji ya serikali miaka yote yamekuwa makubwa kuliko mapato na hata ukiangalia Bunge letu tukufu linakaa linapitisha bajeti, ni juzi limepitisha bajeti ya mwaka 2019/20, lakini ukiangalia mwisho wa mwaka, makusanyo hayaendani na bajeti iliyopitishwa.

"Kwa hiyo, sisi tunafikiri kwamba ni jukumu la Watanzania wote kukaa na kutafakari ni nini kifanyike ili kuiongezea nguvu serikali uwezo wa kukusanya mapato mengi zaidi katika mapato yatokanayo na kodi na mapato ambayo hayatokani na kodi. Ni jukumu la Watanzania wote kwa sababu, serikali inahitaji pesa nyingi kwa ajili ya maendeleo."

Katika ripoti zake zilizozinduliwa jana, pamoja na mambo mengine, Wajibu inasisitiza umuhimu wa maofisa masuhuli kutekeleza mapendekezo ya CAG na maagizo ya Kamati za Kudumu za Bunge ili kujenga uwajibikaji na utawala bora nchini.

Washiriki walioalikwa katika uzinduzi huo ni viongozi wa serikali, taasisi na mashirika yasiyo ya kiserikali na baadhi ya wataalamu kutoka vyuo vikuu.

# Mwili wakutwa kichakani umekatwa miguu, mkono

INATOKA UK. 3

hawezi kutambulika kwani unaonekana una siku tatu au mbili nyuma," alisema Mgoyi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Kamishna Msaidizi (ACPO Richard Abwao, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kwamba mtu huyo ambaye hajafahamika aliuawa na watu wasiojulikana na kisha kutelekezwa polini.

Kamanda Abwao alisema baada ya wauaji kutekeleza tukio hilo, mwili huo waliusambaratisha kwa kuukata vipande vipande na kubakiza kichwa, mkono mmoja na kifua, huku viungo vingine kuanzia kiuno na miguu yake na mkono walitoweka navyo kwa lengo wanalofahamu wao.

Kutokana na tukio hilo, Abwao alisema Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga linaendesha msako ili kuwabaini watuhumiwa wa mauaji, huku akiwasihi wananchi lililokotokea tukio hilo, kuwa wepesi kutoa taarifa ili kudhibiti matukio ya namna hiyo.

Alisema mwili huo umekaa siku nyingi vichakani kutokana na wananchi kutotoa taarifa mapema hali ambayo imesababisha umeharibika vibaya na kichwa kubakia fuvu tu na kusababisha wananchi washindwe kuutambua.

Kamanda Abwao alisema hadi sasa hakuna mtu aliyekamatwa kwa kuhusika na tukio hilo la mauaji.

# Waiomba serikali iache kutoza kodi kwa dola

**Na Allan Isack,** MANYARA

WAFANYABIASHARA wadogo wa madini katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani, Simanjiro mkoani Manyara, wameiomba serikali iwaruhusu kulipa leseni na tozo mbalimbali za madini kwa fedha za Kitanzania badala ya Dola ya Kimarekani.

Wakizungumza kwa niaba ya wafanyabiashara wengine, Hamboya Elia, Hussein Ramadhani, Philemon Samson na Dories Emmanuel, walisema kulipa leseni na tozo za madini kwa kutumia dola ni changamoto inayowakabili hao kutokana na kuwa na mitaji midogo.

Walisema kutokana na kushuka kwa thamani ya shilingi, wanapolipia leseni na tozo za madini kwa dola, wanajikuta wanalipa fedha nyingi ambazo wafanyabiashara wadogo hawawezi kuzimudu.

"Tunaiomba serikali leseni na tozo za madini tuzilipie kwa shilingi na si kwa mfumo wa dola kwa sababu fedha hiyo inaongezeka thamani siku hadi siku, hivyo wafanyabiashara wanajikuta wakilipa fedha nyingi kwa dola na wakati mitaji yao bado ni midogo," alisema Samson.

Walisema walisema changamoto nyingine ambayo serikali inapaswa kuifanyia kazi kwa haraka ni ya wafanyabiashara kuchukua muda mrefu wakati kufanyiwa tathmini ya madini.

"Wafanyabiashara wanapofika sehemu ya kufanyiwa tathmini ya madini wanachukua muda mrefu, hivyo tunaiomba Wizara ya Madini, kutatua changamoto hii kwani inaweza kuwa kikwazo kitakachoikosesha serikali mapato," alisema Elia.

Licha ya changamoto hizo, walisema miundombinu ya barabara ya soko la madini si rafiki, hivyo wakaiomba serikali kuiboresha hiyo, kwa sababu inaweza kuwa chanzo cha ajali zitakazohatarisha maisha ya wafanyabiashara hao.

Ofisa Madini Mkazi wa Wilaya ya Simanjiro, Daudi Ntalimu, alisema suala la wafanyabiashara hao kulipia leseni na tozo za madini kwa dola, limeshatolewa taarifa wizarani na serikali inalifanyiwa kazi baada ya muda watapewa majibu. "Wafanyabiashara wanalalamika kulipia leseni kwa dola wakati wao ni Watanzania. Lakini napenda kuwakumbusha kuwa mfumo huo ulikuwapo tangu mwanzo na serikali haikutambua kuwa ungekuwa na changamoto kwa baadhi ya wizara zake, hivyo tumetoa taarifa kwa mamlaka husika wanalifanyia kazi," alisema Ntalimu. Kuhusu changamoto ya wafanyabiashara kutumia muda mwingi wakati wa kuthaminiwa madini, Ntalimu alisema wameongeza meza nyingine ya uthaminishaji madini pamoja na watumishi.

Pia alisema katika kukabiliana na changamoto ya wafanyabiashara kukaa kwenye foleni kwa muda mrefu, wameongeza siku za kazi ya uthaminishaji wa madini kutoka siku mbili hadi tano kwa wiki.



Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa wa Kimadini wa Simanjiro, Daudi Ntalima, akizungumza na wachimbaji wa madini ya Green kwenye machimbo ya Lemshuku jana. **PICHA: GIFT THADEY**

# Shirika la Maendeleo latoa elimu ya utalii

**Na Zanura Mollel**, ARUSHA

SHIRIKA la Maendeleo ya Jamii Oikos linalofanya kazi wilayani Longido katika Tarafa ya Enduiment chini ya ufadhili wa Umoja wa Ulaya, limewezesha mafunzo ya utalii kwa wanajumuiya wa Enduiment.

Mafunzo hayo ya siku nne, yanafanyika katika kijiji cha Lerangwa kata ya Olmolog ili kukuza uelewa wa masuala ya uhifadhi.

Ofisa Utalii kutoka shirika hilo, Emanuel Tarangei, alisema katika kuboresha shughuli za utalii ndani ya jumuiya hiyo, wanatarajia kukabidhi baiskeli ambazo zitatumika katika shughuli za utalii.

"Tunaamini baada ya mafunzo haya wanajamii wa Enduiment watafahamu masuala ya uhifadhi na faida zake na kuwa mstari wa mbele katika kutunza rasilimali za taifa," alisema.

Alisema wanatoa pia elimu juu ya utalii wa punda kwa kuwa katika hifadhi ya Enduiment kuna maeneo mengi ambayo magari hayawezi kufika, hivyo usafiri wa punda utasaidia wageni kufika maeneo ambayo gari haliwezi kufika.

"Punda watatumika kubeba mizigo huku wageni wakitembea kwa miguu na kujionea mazingira ya hifadhi hiyo," alisema Tarangei.

Aidha, alisema hifadhi ya Enduiment ni ya kipekee na tofauti kwa kuwa wanyama wa aina mbalimbali wapo na mazingira ya hifadhi ni mazuri, hivyo wamelenga kutoa elimu ili jamii ifahamu umuhimu wa uhifadhi na faida zake. Mmoja wa wanufaika wa mafunzo hayo, Magdalena Lengay,

Mkazi wa Kijiji cha Lerang'wa, alisema mafunzo hayo yamewanufaisha, japo wanawake wa jamii ya Kimasai wengi wao hawapewi fursa na waume zao katika kufanya shughuli za utalii ikiwamo ushonaji wa shanga.

Magdalena alisema jamii ya kifugaji inategemea kuwezeshwa kwenye vyanzo vya mapato na waume zao, lakini changamoto kubwa inayowakabili ni waume zao kuwanyima fedha za kuwekeza kwenye fursa za kitalii.

Alikemea kuwapo kwa wanawake wa jamii hiyo kubweteka kwa kuacha kubuni njia za kujipatia kipato, ikiwamo wale wanaouza shanga walizovaa mwilini kwa matamanio ya fedha.

# EALA na Misa- Tan kukuza uhuru habari

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SPIKA wa Bunge la Afrika Mashariki (EALA), Martini Ngoga, ameahidi kufanya kazi na wadau wa habari nchini, ili kuboresha mazingira ya uhuru wa vyombo vya habari na upatikanaji wa taarifa nchini na eneo la Afrika Mashariki kwa ujumla.

Ahadi hiyo alitoa juzi katika makao makuu ya jumuiya hiyo, mjini hapa wakati akizungumza na wajumbe wa Bodi ya Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika (MISA) Tawi la Tanzania.

Wajumbe hao wa Bodi ya Misa-Tan, walimtembelea Spika Ngoga ofisini kwake na baadaye kualikwa bungeni na kuzungumza na wabunge wawakilishi wa Tanzania kwenye bunge hilo.

Spika Ngoga alisema uhuru wa habari, uwazi na ukuzwaji demokrasia ni moja ya mambo ambayo yamo katika mkataba wa kuanzishwa jumuiya hiyo, hivyo watashirikiana na wadau kupitia Misa- Tan kusaidia kukuza uhuru huo lakini kwa kuzingatia maadili ya uandishi. Alisema kumekuwapo na tatizo katika utendaji wa vyombo vya habari katika ukanda wa Afrika Mashariki, kuandika mambo mabaya tu katika nchi hizo, badala ya kuandika pia mambo mazuri ynayofanywa ili kuwatia moyo viongozi na wananchi.

"Si kama hatutaki muandike mabaya, hapana, bali tunataka mjirekebishe kwa kuandika hata masuala mazuri ili kuzitia moyo serikali na wananchi waliomo katika nchi hizo wanachama," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Misa-Tan, Salome Kitomari, alisema malengo ya taasisi hiyo ni kukuza uhuru wa habari na uhuru wa kujieleza nchini na kutaka EALA kusaidia ukuaji wa tasnia ya habari nchini.

Alisema kuna baadhi ya vifungu vya sheria vilivyopitishwa katika nchi wanachama wa jumuiya hiyo, vinaathiri utendaji wa vyombo vya habari, ikiwamo sheria ya takwimu, sheria ya huduma ya vyombo vya habari na makosa ya mtandao.

Mjumbe wa Bodi hiyo, Mussa Juma, alimweleza Spika huyo kuwa Misa- Tan inaliomba Bunge hilo, kuimarisha uhusiano na vyombo vya habari, ikiwamo kushirikiana kuwepo sheria katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, ambazo zitasaidia kukuza uhuru wa vyombo habari.

# Walia waajiri kutopeleka fedha NSSF

**Na Mary Mosha,** SIHA

CHAMA cha Wafanyakazi wa Mashambani na Kilimo (TPAWU), kimeiomba serikali kuingilia kati tatizo la kukatwa fedha na waajiri lakini hazifikishwi kwenye mifuko ya hifadhi wa jamii (NSSF) kwa wakati.

Hayo yalisemwa na mmoja wa viongozi wa chama hicho wakati akizungumza kwa niaba ya wafanyakazi wenzake kwenye mkutano mkuu wa kamati ya utendaji kanda ya Kilimanjaro.

Mwenyekiti wa TPAWU, tawi la Relongo Estate, lililoko Wilaya ya Siha, Rashid Mswaki, alifafanua kuwa waajiri hao wamekuwa wakiwakata fedha hizo kwa ajili ya mifuko mbalimbali ya kijamii ikiwamo NSSF, ilhali hawaziwasilishi kwa wakati.

Mswaki aliiomba serikali na uongozi wa TPAWU, ziingilie kutatua tatizo hilo ambalo limegeuka kuwa mwiba kwa ustawi wa kiuchumi kwa kazi zao na familia zao pia. Elias Mashamba Mwenyekiti wa TPAWU, tawi la TPC alisema changamoto kubwa iliyoko kwa wafanyakazi, wanapoumwa wakienda kutibiwa hospitalini hawapati huduma hiyo kwani fedha wanazokatwa hazikuwasilishwa na waajiri.

"NSSF ni wadau wakubwa kwa wafanyakazi wa mashambani, wanapata mapato mengi kupitia kwetu wafanyakazi wanapoumwa wanastahili fao la matibabu, lakini tunapokwenda kupata huduma hiyo ambayo ni stahili yetu tunaambiwa mchango haujatosha kwa kweli inakatisha tamaa," alisema Mashamba.

Suzan Nkini, Mwenyekiti wa Vijana TPAWU, Kanda ya Kilimanjaro aliiomba serikali isaidie kuzibana taasisi ambazo zinashindwa kupeleka michango ya wafanyakazi wao kwa wakati

Akisoma taarifa ya mwaka Katibu wa TPAWU Kanda ya Kilimanjaro, Hatibu Losiando, alifafanua kuwa chama hicho kimeongeza kiwango cha makusanyo kwa mwaka kutoka milioni 35 mwaka 2014 hadi kufikia milioni 120 kwa sasa 2019.

Losiando alisema kuwa pamoja na mafanikio hayo TPAWU Kanda ya Kilimanjaro inakabiliwa na changomoto mbalimbali ikiwamo ukosefu wa gari la kuwafikia wakulima mashambani hasa kwenye maeneo ya vijijini, pamoja na samani za ofisi hali ambayo inakwamisha utendaji kazi. Kwa upande wake Mwenyekiti wa TPAWU Kanda ya Kilimanjaro, Juma Mdolo, aliwataka waajiri kuendelea kuwapa fursa wafanyakazi kupata ujuzi ili kujenga uhusiano baina ya wafanyakazi na waajiri.



Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira (kulia), akikabidhi Mwenge wa Uhuru kwa Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Martine Shigela, katika eneo la kijiji cha Bwiko, wilayani Korogwe, kwa ajili ya kuanza mbio zake mkoani humo juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Rombo, Moshi Mjini zaongoza ukatili kijinsia

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

TAKRIBANI kesi 150 za masuala ya ukatili wa kijinsia zimekuwa zikiripotiwa kwa kipindi cha miezi sita katika dawati la jinsia na watoto mkoani Kilimanjaro.

Aidha, Manispaa ya Moshi Mjini na Wilaya ya Rombo zinaongoza kuwa vinara wa makosa hayo.

Mkuu wa dawati hilo mkoani Kilimanjaro Zuhura Suleyman, alisema hayo kwenye mafunzo yalitolewa kwa waendesha mashtaka, polisi, mahakimu na maofisa ustawi wa jamii mjini Moshi.

Wilaya za Hai na Same zimekuwa na matukio machache ya ukatili ikilinganishwa na wilaya nyingine, kwa mujibu wa maelezo yake.

Alisema tatizo hilo linatokana na asilimia kubwa ya wazazi kutumia muda mwingi kufanya shughuli za kiuchumi na watoto wakiachwa na wazee au walezi nyumbani.

Mafunzo hayo yaliyoandaliwa na Shirika la Kilimanjaro Women Information Exchange Community Organization (Kwieco) na Asasi ya Crossroads International kutoka Canada, yanalenga kuwapa uelewa wa jinsi ya kukabiliana na ukatili huo.

Wakati wa mafunzo hayo, mkuu wa dawati, alieleza kuwa makosa ni mengi kwenye masuala ya ukatili, tunapokea kesi nyingi za watoto za kunyanyaswa, kubakwa na kwa wanawake kesi nyingi zinaelekezwa kwenye kutelekezwa.

Alisema changamoto kubwa ni jamii kukosa ushirikiano licha ya kesi nyingi lakini wahanga wanabadilika na kuharibu ushahidi kwa kuongea na mtuhumiwa kumaliza kesi nyumbani.

Mohamed Seif, Ofisa Ustawi wa Jamii Manispaa ya Moshi, alisema kumekuwa na changamoto kubwa katika mabadiliko ya jamii na kupeleka vitendo vya uvunjifu wa sheria na ukatili kwa wanawake na watoto.

Alisema katika kupambana na changamoto ya ukatili wa kijinsia wanakabiliwa na matatizo ya pengo kubwa la ushirikiano baina ya familia na taasisi zinazoshughulikia ukatili wa kijinsia.

"Hapa tunaongelea watu wenye taaluma tofauti kuanzia Jeshi la Polisi, maofisa ustawi wa jamii taasisi zisizokuwa za kiserikali, mawakili na majaji na wananchi hili jukumu linaanzia ngazi ya familia."

"Kabla ya programu hii ya Access to Justice haijafika hapa Moshi kulikuwa na vikwazo vingi katika kupambana na suala hili, kulikuwa hakuna ukaribu ulikuwapo mpaka kati ya ofisa ustawi wa jamii na mahakimu kwa vile ni mihimili tofauti. Lakini kwa sasa ni kama imekwisha," alisema.

Watoto wamekuwa wakibakwa na kulatiwa ndizo kesi nyingi zinazopokelewa baada ya kuelewa nafsi yetu tumekuwa bega kwa bega kuwapa ujasiri ili waweze kueleza kile kinachotakiwa mahakamani.

Hakimu Mkazi wa Wilaya ya Siha, Jasmine Abdul, alisema kuna changamoto ya masuala ya makosa ya unyanyasaji wa kijinsia katika sheria kwani wahusika hasa wazazi na walalamikiwa wanafanya mkutano kabla ya kesi kujali kutokuwapo kwa shahidi mahakamani.

"Sheria zetu zinatubana kufanya maamuzi kama shahidi hajafika mahakamani inatupasa kuondoa kesi hiyo hatutakiwi kukaa na kusema shahidi atakuja. Tulichojifunza kutokana na kesi hizi tunatakiwa kuwa wavumilivu tusibanwe sana na sheria hadi kukwamisha haki," alisema Hakimu Abdul.

# Vijana waunda mitambo, roboti

**Na Mary Mosha,** SAME

KATIKA kuunga mkono serikali kufanikisha juhudi za vijana kujiajiri pamoja na kutekeleza sera ya viwanda, taasisi za dini zimeanza kuwapa wanafunzi mafunzo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama) kwa vitendo ili kujiingiza kwenye uwekezaji wa viwanda na kujiajiri.

Mafunzo hayo yanayotolewa kwa wanafunzi zaidi ya 30, wanaotokea katika shule za msingi, sekondari na vyuo vikuu yanawawezesha kufundishwa namna ya kutengeneza mitambo na mashine mbalimbali zikiwamo za kukata majani bila msaada wa mwanadamu.

Aidha, wanatengeneza roboti kwa ajili ya kuzituma sehemu mbalimbali kuzima moto na kusaidia shughuli nyingine za kilimo.

Akimkaribisha Mkuu wa Wilaya ya , RoseMary Sinyamule, kwenye mafunzo hayo yanayoendelea huko Same, Mchungaji wa Kanisa la Kipentekoste Tanzania (TAG) Same mjini, John Munisi, alisema wanashirikiana na Shirika la Empower One Empower Village kuwasaidia vijana wa Same wanaotoka kwenye mazingira magumu ili wawe chachu ya maendeleo wilayani humo.

Alisema wanafunzi hao wanatoka katika usharika wa dini mbalimbali wakiwamo wa kanisa la Kilutheri, Anglikana na Kipentekoste ambayo kwa ushirikiano huo, wanapata mafunzo bila malipo.

Aidha, wanawafuatiliwa mara kwa mara wanapofanikisha mabadiliko hasa ya kielimu.


"Pamoja na mafunzo tunayowapatia lakini wametengeneza mtandao ambao unabeba vitabu vyote muhimu ili kujifunza na kufanya vyema katika masomo yao."

Aliiomba serikali kuwaunga mkono ili waweze kuonyesha vipaji vyao kwa vitendo katika taifa hili linalojitahidi kuondoa umaskini na ukosefu wa ajira.

Akifunga mafunzo hayo Mkuu wa Wilaya ya Same alisema ni dhahiri kuwa watoto hao wamepata mwanzo mzuri utakaowasaidia kupiga hatua katika maisha ikiwa watatumia vyema elimu waliyoipata.

Alisema kwa sasa dunia inategemea teknolojia kwa hali zote, hivyo, kuwaomba vijana kuwa chachu ya mabadiliko hayo kwa kuleta maendeleo na sio vinginevyo.





Kaimu Mkurungenzi Mkuu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Gilbert Chawe (kulia), akipokea hati ya shukrani kutoka kwa Waziri Mkuu Kasimu Majaliwa, kwa kutambua mchango wa mfuko huo katika kudhamini Kongamano la Uwekezaji Mkoa wa Dodoma lililofanyika jijini humo juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# CAG Assad azipa somo Azaki

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, amezitaka asasi za kiraia kuhakikisha zinasaidia kulinda rasilimali za asili ambazo zimekuwa zikitumika vibaya.

Prof. Assad alitoa rai hiyo jana jijini hapa alipofungua mafunzo ya kuhusu madini, mafuta na gesi yanayotolewa kwa wadau 80 kutoka asasi mbalimbali zisizo za serikali.

Alisema lengo la mafunzo hayo ni kupata uelewa katika eneo hilo jipya la sekta ya madini, mafuta na gesi ili kusaidia kulinda rasilimali hizo.

"Rasilimali zetu za asili zimekuwa zikitumika vibaya hasa nyakati hizi, hivyo kila mmoja wetu anafahamu ubadhirifu unaoendelea katika nyanja mbalimbali zinazohusu sekta ya madini, mafuta na gesi. Mafunzo haya yatatusaidia kuelewa na kuzilinda rasilimali hizi," alisema.

Prof. Assad alisema mafunzo hayo yamefadhiliwa na Benki ya Dunia (WB) kwa kushirikiana na ofisi yake ili kuhakikisha wadau hao wanapata mafunzo ya kuwajengea uwezo wa uelewa wa sekta hiyo.

"Wawezeshaji wetu ni kutoka taasisi ya KPMG ambao ni wataalamu kwenye maeneo haya ya madini, mafuta na gesi, na wataendesha mafunzo haya kitaalamu kusaidia kuongeza thamani na tija," alisema.

CAG Assad aliwataka wadau hao kushiriki kikamilifu ili kila mmoja kupata uelewa wa kina ambao utawasaidia kwenye majukumu yao.

Wakizungumza kwenye mafunzo hayo, baadhi ya wadau walisema mafunzo hayo ni muhimu yakashushwa ngazi za chini ili Watanzania wawe na uelewa wa kutosha wa kulinda rasilimali hizo.

Akitoa mada kuhusu sekta ya gesi na mafuta, mbia wa KPMG Tanzania, Alexander Njombe, alisema Tanzania kuna gesi futi za ujazo trilioni 57.54 ambazo zinaweza kutumika miaka 50 bila kuisha. Alisema kuwa kati yake, futi za ujazo trilioni 10 ziko sehemu ya nchi kavu.

# Wazalishaji bidhaa kukutana na Waziri Bashungwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, ameandaa kikao na wazalishaji wa bidhaa mbalimbali nchini kwa lengo la kujua changamoto zinazowakabili na kuzitatua. Katika kongamano la uwekezaji fursa lililofanyika jijini hapa juzi, waziri huyo alisema mbali na kutaka kujua changamoto, serikali inahitaji kujua hali ya uzalishaji na ajira zilizopo.

"Natarajia kuandaa kikao na wazalishaji wa bidhaa mbalimbali, lengo ni kutaka kujua wapi wanakwama katika uwekezaji wao," Bashungwa alisema.

Waziri huyo alisema kongamano hilo limesaidia wawekezaji kujua fursa zilizoko katika Mkoa wa Dodoma na kuagiza kuendelea kuandaa makongamano yatakayohamasisha uwekezaji.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, alisema katika kuimarisha uwekezaji, jumla ya ekari 12,090 za ardhi zimetengwa na jiji hilo jipya kwa ajili ya uwekezaji. Dk. Mahenge alisema tayari Kituo cha Uwekezaji kimefungua ofisi ya Kanda ya Kati ili kurahisisha mchakato mzima wa uwekezaji kwa wawekezaji.

Alibainisha kuwa katika kipindi cha kuanzia Julai 2016 hadi Juni mwaka huu, TIC imesajili jumla ya miradi 22 jijini, ikitarajiwa kuwa na mtaji wa Dola za Marekani milioni 232.51 na kutoa ajira 2,867.

Dk. Mahenge pia alibainisha kuwa mpaka sasa, uzalishaji wa umeme katika jiji hilo umefikia MW 48, wakati matumizi yake ni MW 28 na kwamba kati ya vijiji 304 vilivyoko katika mkoa huo, 593 tayari vimeunganishwa na huduma ya umeme kupitia Mradi wa Nishati Vijijini (REA).

# 'Blue print' kuanza mwezi ujao

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali itaendelea na utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji (The Blue Print) utakaoanza Julai Mosi, mwaka huu.

Majaliwa aliyasema hayo juzi alipofungua kongamano la fursa za uwekezaji la mkoani Dodoma kwa niaba ya Rais John Magufuli.

Alisema serikali itaendelea kushirikiana na sekta binafsi katika kuweka mazingira wezeshi ya kuvutia uwekezaji na biashara nchini.

Waziri Mkuu alisema mpaka sasa, hatua mbalimbali zimeendelea kuchukuliwa kwa lengo la kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji na biashara nchini.

"Miongoni mwa hatua hizo ni uwapo wa usafiri wa uhakika na wa haraka wa abiria na mizigo kwa kujenga reli ya kiwango cha kimataifa," alisema.

Waziri Mkuu alisema Uwanja wa Ndege Dodoma pia umeboreshwa na kuruhusu ndege kubwa na ndogo kutua usiku na mchana.

Alisema mashirika ya ndege yanayotoa huduma yameongezeka na maandalizi ya awali ya ujenzi wa uwanja wa kimataifa wa ndege katika eneo la Msalato yanaendelea.

Waziri Mkuu alisema Mkoa wa Dodoma una barabara za kuaminika za kiwango cha lami zinazoiunganisha na mikoa mingine pamoja na nchi jirani.


Alisema serikali ya awamu ya tano imeendelea kuboresha huduma za afya na Dodoma kuna hospitali ya Benjamin Mkapa.

Awali, Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, aliwataka wawekezaji kuchangamkia fursa kwenye sekta ya kilimo kwa kujenga viwanda vya kuongeza thamani ya mazao 85 nchini ili kukifanya kilimo kuwa na tija.

Hasunga alisema kuna fursa mbalimbali za uwekezaji katika kilimo ambazo bado zinahitaji wawekezaji kama vile viwanda vya mbolea, viwanda vya kuongeza thamani ya mazao mbalimbali na viuatilifu.

"Tunahitaji kupata wawekezaji katika suala la uongezaji thamani kwenye mazao yetu 85 nchini ili kukifanya kilimo chetu kuwa na tija," Hasunga alisema.

Naye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa (Tamisemi), Selemani Jafo, aliagiza mikoa ambayo haijaandaa makongamano ya kutangaza fursa za uwekezaji, kufanya hivyo haraka.





# Walimu waanzishiwa idara ya Tehama

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, imeanzisha Idara ya Habari ya Teknolojia na Mawasiliano (Tehama)kusaidia walimu kufundisha masuala ya teknolojia.

Mkurugenzi wa Mafunzo ya Elimu Zanzibar, Maimuna Fadhil Abbas, amesema hayo wakati akifungua uzinduzi wa mafunzo kwa walimu 25, wa mikoa mitano ya Zanzibar.

Mkurugenzi Abbas, alisema elimu hiyo itawasaidia walimu kutumia njia za kisasa badala ya kutumia vitabu pekee.

Alisema Tehama ina umuhimu mkubwa katika ufundishaji kutokana na kutumia njia ya mtandao na wanafunzi kupata elimu juu ya matumizi sahihi ya mtandao.

Aidha, aliwahimiza walimu hao kuwafundisha wanafunzi njia sahihi ya matumizi ya teknolojia kutokana na baadhi yao kushindwa kutumia mitandao kwa kupata elimu.

Alishukuru hatua ya Shirika la kiraia la Shule Direct lililoonyesha kuunga mkono jitihada za serikali katika sekta ya elimu nchini.

"Naamini kwamba kupitia mafunzo haya kwa walimu wetu wa sayansi utakuwa ni mwanzo mzuri wa kuongeza idadi kubwa ya wanafunzi wanaopatiwa elimu ya Tehama ambayo ni muhimu wakati huu wa kuelekea uchumi wa viwanda," alisema Abas. Aliongeza kuwa katika juhudi za serikali ya Zanzibar kwenye uimarishaji wa masomo ya teknolojia, wameanzisha masomo ya Tehama kwa wanafunzi kuanzia darasa la tano, ambayo yana lengo la kuona watoto hao wanaimarika zaidi kielimu kwenye mawasiliano.

Alisema hatua nyingine ni kuwageuza baadhi ya walimu wa masomo ya sanaa kuwa walimu wa masomo ya sayansi, lengo likiwa ni kuona walimu hao wanakuwa msaada wa ufundishaji wanafunzi katika madarasa mbalimbali.

Aidha, Meneja wa Shirika la Shule Direct, Ikuu Lazaro, alisema zaidi ya wanafunzi 1,500,000 kutoka shule mbalimbali za Zanzibar pamoja na baadhi ya mikoa ya Tanzania Bara wamepatiwa mafunzo hayo. Alisema idadi hiyo ya wanafunzi inatokana na uongozi wa shirika hilo kuzifikia shule 80 kwa baadhi ya mikoa ya Tanzania Bara na Zanzibar kupitia mfumo wa kujifunzia unaopatikana bila matumizi ya mtandao ambao tayari umeshahifadhiwa ndani ya shule hizo.

Alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwaandaa wanafunzi katika kuelekea uchumi wa viwanda ambao ni miongoni mwa vipaumbele vya serikali.

"Tuna zaidi ya walimu 30,000 ambao tumewapatia mafunzo ya Tehama ambao nao wana wajibu wa kueneza elimu hiyo kwa wanafunzi..."

Kwa upande wa mtoa mada wa mafunzo hayo, Saada Salim alisema umoja na ushirikiano na walimu hao ni moja ya mafanikio ya mafunzo hayo yanaendeshwa chini ya Shirika la Shule Direct la Tanzania.

Walimu walioshiriki mafunzo hayo wameahidi kutekeleza kwa vitendo elimu watakayopatiwa ili kuleta mageuzi makubwa katika ufundishaji wao wanaporudi shuleni.



Mwenyekiti wa Kamati ya Uongozi ya Ofisi ya Mpango wa kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge (Mkurabita), Balozi mstaafu Daniel Ole Njolay (wa pili kulia), akikabidhi hati ya ardhi kwa Mkazi wa Mpendae, Said Yahya, katika hafla iliyofanyika huko Mpendae, mjini Zanzibar juzi. Kulia ni Mrajisi wa Ardhi Zanzibar, Dk. Abdul-Nasser Hikmany. **PICHA: MAELEZO**

## Taasisi zahitaji lugha ya alama

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa Mjini Magharibi Ayoub Mohammed Mahmoud, ameshauri taasisi zinazohusika na haki na sheria kujifunza lugha ya alama.

Aidha, Jeshi la Polisi, Mahakama, na Ofisi ya Mwendesha Mashtaka (DPP), ndizo taasisi zilizoshauriwa kuwa na wataalamu wa lugha ya alama, ili kusaidia katika masuala ya ushahidi na uwendeshaji wa kesi kwa watu wenye ulemavu na viziwi.

Aliyasema hayo wakati akifungua mkutano wa wadua kuhusu ushawishi na utetezi kwa watu wenye ulemavu uliofanyika Zanzibar.

Aliwashauri wasimamizi wa mradi wa ushawishi na utetezi wa lugha ya alama kuihusisha Ofisi ya Mwendesha Mashtaka na Kituo cha Huduma za Sheria kwa kuwa taasisi hizo ndizo zinazohusika na masuala hayo.

Alisema hatua hiyo itasaidia pia kuwaunganisha kwa karibu watu wenye ulemavu wa uziwi na wahusika wa haki za jinai katika mambo ya kisheria.

Aidha, alisema kwamba Mkoa wake utaendelea kuunga mkono mikakati mbalimbali ya watu wenye ulemavu ili kuweza kufikia malengo waliyokusudia.

Mratibu wa mradi wa ushawishi na utetezi wa lugha za alama Jide Khamis Saleh, alisema lengo la mradi huo ni kutoa mafunzo ya utetezi wa lugha za alama kwa vyombo vya ulinzi na usalama na mahakama kutokana na mwamko mdogo wa lugha hiyo kwa vyombo hivyo.

Alisema taasisi nyingi zimekuwa zikielekeza miradi yao katika maeneo ya mjini, lakini jumuiya yao imeamua kutekeleza mradi huo Mkoa wa Kaskazini Unguja.

# Makamu wa Rais Zanzibar ahimizi kulinda utamaduni

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amesema kulinda utamaduni wa nchi ni sawa na kulinda rasilimali muhimu za taifa.

Alisema hayo katika sherehe za kushajihisha mpango wa nchi yetu ni urithi wetu ikiwa ni miongoni mwa sherehe za Maadhimisho ya Skauti ya Duniani ya kutimiza miaka 107.

Katika sherehe hizo zilizofanyika katika mjini Unguja, hotuba yake ilisomwa na Waziri wa Vijana, Utamaduni Sanaa na Michezo, Balozi Ali Abeid Karume.

Alisema kulinda utamaduni ni miongoni mwa vielelezo vinavyotumika kutofautisha taifa moja na jingine duniani.

Alisema utamaduni ni tasnia muhimu katika kulinda heshima ya taifa lolote, hivyo ni vyema wazazi kushirikiana na walimu ili kuhakikisha watoto wanafundishwa masuala ya mila, silka na utamaduni ili waweze kuzitambua na kuacha kuiga tamaduni za kigeni.

Aidha, alisema kuboresha Skauti nchini ni miongoni mwa mbinu bora za kulinda utamaduni wa nchi kwa kuheshimiana na kuthaminiana pamoja kuwajenga vijana kuwa wazalendo, wa kulinda na kutetea nchi yao.


Aidha, aliwataka vijana wa skauti kuendeleza ushirikiano na upendo bila ya kuwepo viashiria vya ubaguzi wa hali yoyote kati yao na vijana wengine, ili kuidumisha amani na utulivu uliopo katika taifa hili.

Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohammed Said, alisema ipo haja ya kuipa jamii elimu juu ya kutunza urithi wa nchi kama mavazi, pamoja na kudumisha mila, silka zilizopo ili kuwasaidia watoto kuwa na maadili mema ambayo yatasaidia kutokomeza vitendo vya udhalilishaji nchini.

Kwa upande wake Skauti Mkuu Tanzania, Mwantum Bakar Mahiza, alisema, hivi sasa jamii imetawaliwa na utandawazi unaosababisha kuporomoka kwa maadili, hivyo, ipo haja ya vijana kupata stadi zitakazopelekea kuwa watoto wema.

Mkurugenzi wa Idara ya Michezo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Zanzibar, Hassan Tawakali Khairalla, alisema ushajihishaji huo ni mpango maalum ulioandaliwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, ambao umelenga kuwakuza vijana kuwa na maadili mema.

Kauli mbiu katika sherehe za kutimiza miaka 107 ya Skauti Duniani ni "Nchi yetu ni urithi wetu".




Soma UK. 16

**CHILO**

JUMAMOSI JUNI 29, 2019

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE



# UTANASA KAMA SUMAKU

UK.14

## BASI SAWA



# PMM waanza na Go Down

STUDIO mpya ya PMM ya Sinza Dar es Salaam, imeanza kuwatambulisha wanamuziki wake na kwa kuanzia imeachia singo kali inayoitwa 'Go Down' kutoka kwa msanii aitwaye Finally.

Kwa mujibu wa meneja wa studio hiyo Prosper Kiri alisema lengo la kutambulisha wasanii hao ni kutaka kutoa salamu kwamba wanakuja kutikisa muziki wa Bongofleva nchini.

"Baada ya kutambulisha Go Down tunaendelea kurekodi kazi zingine chini ya maprodyuza Gerry Beats pamoja na Sammily (Dr Dre)," amesema.




# Jux, Vanessa wanasana kama 'Sumaku'

WAKATI uvumi unasambaa kuwa wanamuziki walio kwenye mapenzi, Jux na Vanessa Mdee, mambo hayaendi sawa, wawili hao wametambulisha ngoma yao kali.

Wimbo huo unaoitwa 'Sumaku' wasanii hao wamejikuta wakiimba kwa hisia na kutaja mambo ambayo kila mtu anavutika kutoka kwa menzake. Sumaku wimbo ambao umetengenezwa na S2kizzy umeonekana kufuta dhana hiyo na kusababisha mashabiki kuona hali hiyo ilitengenezwa kwa makusudi ili kuwaweka tayari na singo mpya.



# 4U & Mr Blue habari ya mjini na 'Nimwage Maji'


MSANII wa muziki wa kizazi kipya Bongo Fleva, Fadhil Yusuph '4U', alisema ngoma yake mpya ya 'Nimwage Maji', imetendewa haki na Mr Blue, ambaye alimshirikisha.

Akizungumza hivi karibuni, 4U amesema kibao hicho anaamini itafanya maajabu kwenye muziki wake kutokana na kuwa tofauti.

"Nahitaji kufanya mambo makubwa zaidi, mashabiki wangu waniamini katika hili, pia nashukuru Mr Blue amefanya kazi kubwa ndani ya hii ngoma, naomba sapoti kubwa zaidi kutoka kwa Watanzania," alisema 4U.

## INSTA-TWITTER





**Hivi** unataka na mimi nifungashe nyonyo kama hizi kha! Hii si adhabu hii loh! Nyonyo bado kidogo lifike kidevuni kha!- **Faiza Ally**.



**Wabongo** bwana. Sasa hasira mkahamishia kwa dogo (aliyetufunga goli la pili) Kosa lake nini? Kupiga ile mashine? Mlitaka afanyaje? Kwa taarifa yenu dogo ni bebi wa mtu na anaishi Masaki ya Ubelgiji karibu kabisa na nyumba ya Bakhresa wa huko - **Edo Kumwembe**



## Bella amkana Hamisa Mobetto

MWANAMUZIKI mkali wa Bongo Fleva, Christian Bella, wanaosema yeye anatoka kimapenzi na mwanamitindo Hamisa Mobetto, wameshindwa kumwelewa.

Bella ameiambia EATV, kwamba kauli yake kuwa pindi anapomwona Mobetto anaona sura za watu ambao ameshatoka nao, hakumaanisha wao ni wapenzi.

"Mimi na Hamisa tunafanya kazi pamoja, tupige stori watuombee mazuri, msapoti Hamisa afanye vizuri, tufanye shoo nini na nini, sio waseme mambo ya sita kwa sita," amesema.




**@burudanitele**

**>>> Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow**

## UNASEMAAA...



# SHILOLE mdomo huo utakuponza

MSANII wa muziki na mjasiriamali Zuwena Mohammed maarufu kama "Shilole" amesema mapenzi ya watu mastaa sawa na kuigiza.

Shilole ambaye yupo katika ndoa na mume wake Uchebe, kwa mwaka wa pili sasa, amesema hayo kupitia mahojiano na EATV na EARadio Digital.

"Inategemea mtu anataka mtu wa aina gani, kama mimi nilitaka mtu ambaye sio staa, ili niweze kuishi kwa raha, maana ukiwa na mahusiano na staa mtavimbiana, itakuwa sio sawa, hakuna mapenzi inakuwa mnaleteana maigizo."

## INSTA-TWITTER

Tuffolow/ Tu-tag
**@burudanitele**



**Siku** ya kwanza mgeni anachinjiwa kuku. Siku ya pili anapewa chakula cha kuku. Siku ya tatu na nyingine zinazofuata anaweza kulala alipo kuku **-Dogo Janja.**



**Siwezi** kuishi bila wewe ni kauli ya kinafiki sana kwenye maisha ya mahusiano - **Johari.**



**Kwani** nauli ya kwenda Misri shilingi ngapi nitakulipia ya kwenda mwanangu Ibrahim Ajibu kwani si bado hatujachelewa? - **Tundaman.**

# Kuumbe!



# TUNAWEZA

## MZEE CHILO ANAPOWAMSHA NA KIDIGITALI

**Na Mmwandishi Wetu**

ULIMWENGU wa tasnia ya filamu unaweza kubadilika na kurudi katika mvuto wake wa awali baada ya wasanii kubuni njia mbalimbali za kuinua.

Moja ya watu wanaopambana kurudisha filamu kwenye ubora wake ni Ahemd Olotu, maarufu kama Mzee Chilo ambaye kupitia kampuni anayoiongoza ya Pilipili Entertainment ameanzicha Chanel maalum kwa ajili ya kuonesha kazi mbalimbali za Kitanzania.

Chaneli hiyo inayoitwa MambotvSwahili itaanza kuonekana katika visimbizi tofauti vya hapa nchini.

Gazeti hili liliweza kufanya mahojiano na nguli huyo wa filamu kuhusiana na harakati zake katika ukuaji wa tasnia hiyo.

**BT:** Lengo la kuanzisha chanel hiyo ni nini?

**Mzee Chilo:** MambotvSwahili imenzishwa kwa ajili ya kuwaburudisha na kutoa mafunzo kwa Watanzania kupitia sanaa.

**BT:** Kuna vituo vingi vya Tv vinavyoonyesha filamu za Kitanzania, je, kuna kitu gani kipya kitakachowapa utofauti na wengine?

**Mzee Chilo:** Tumejipanga kuhakikisha tunakidhi kiu ya watazamaji, naweza kusema kila mtu ategemee kuona tamthilia pamoja na filamu mpya na zenye ubora.

**BT:** Unaamini kuanzisha chaneli ya aina hiyo inaweza kuwa mkombozi kwa wasanii?

**Mzee Chilo:** Kwa upande wangu naamini kuwa hivyo, kwani mimi kama msanii mkongwe nimepitia mengi najua mambo yanayoua filamu za Bongo. Kupitia fursa hii itaondoa dhana ya wasanii kudhulumiwa au kuonekana kama ombaomba.

**BT:** Unaamini tasnia ya filamu imeathirika kwa kiasi kikubwa?

**Mzee Chilo:** Kuna mambo mengi yanayofanya watu kuona kama filamu zetu zimepoteza mwelekeo, lakini naweza kueleza kwamba kwa sasa hali imezidi kuimarika na watu wameanza kurudisha mapenzi yao kama huko nyuma.

**BT:** Fursa zikoje kwa wasanii kupitia chaneli yenu mpya?

**Mzee Chilo:** Fursa zipo na wanaruhusiwa kushiriki katika tamthilia zetu zinazofanywa na pilipili pamoja na kuleta kazi zao ili Watanzania wazione. Maudhui na programu zetu kuanzia Jumatatu hadi jumapili kupitia kisimbuzi cha ZMUX.

Nini maoni yako kwa jumla kuhusu wasanii wa tasnia ya filamu?

Mzee Chilo: Sisi tumeanza lakini kuwepo na harakati kubwa ya kuhakikisha filamu ya Kitanzania inaendelea kukua na kuvuka mipaka ya Afrika kama ilivyo kwa Nigeria. Jitihada hizi zitafanywa na sisi wenyewe kwa kushirikiana na serikali na taasisi zingine binafsi.



# BONGO FLEVA WALIOIMBA REGGAE

**Na Adam Fungamwango**

REGGAE ni aina ya muziki maarufu kutoka nchi ya Jamaica na ulianzishwa mwaka 1968 na kuwa maarufu kimataifa kutokana na mwanamuziki Bob Marley na kundi lake la The Wailers.

Awali ulionekana kama ni muziki wa ovyo, lakini Bob Marley aliubadilisha na kuanza kuimbwa kwa mpangilio, huku ujumbe maridhawa kwenye nyimbo hizo uliosababisha kupendwa na watu wa mataifa mbalimbali duniani.

Hata hivyo, aina hii ya muziki hupendwa zaidi na watu wenye imani za rastafari, ingawa kwa sasa umekuwa ukipendwa na watu wengine kama miziki mingine duniani.

Kwa kiasi kikubwa Bob Marley ndiye aliyeutangaza na kuueneza duniani kiasi cha yeye si kuwa maarufu tu, bali kuwa ndiyo nembo ya muziki wenyewe.

Hadi leo umekuwa na wapenzi wengi, kiasi cha hata wasanii wa kizazi kipya pia kuimba baadhi ya nyimbo kwa staili hiyo ya reggae.

**Aslay-Pusha**

MSANII kijana, Aslay Isihaka alishangaza wengi 2017 alipotoa ngoma moja kali iitwayo 'Pusha' ambayo iko katika mtindo wa reggae.

Katika ngoma hiyo, Aslay anamlalamikia kijana mmoja mtaani ambaye ana tabia ya kumzengea mkewe, hivyo anawaambia rafiki zake wamkanye kwani siku akimkuta ole wake na atakufa naye.

Ni ngoma ambayo ilipendwa na watu wengi na kumfanya msanii huyo kuheshimika kwani si rahisi sana kwa wasanii wengi wa sasa kutoa ngoma kwa staili hiyo na ikahiti.

**Galatone-Samaki**

KUNA msanii mmoja anaitwa Galatone. Huyu mwaka 2016, alitoa bonge la ngoma inaitwa 'Samaki'.

Achilia mbali maudhui ya ngoma hii, lakini kuna mchanganyiko wa staili pia.

Ni ngoma ambayo imepigwa katika mtindo wa 'reggae', lakini pia papo hapo hapo inabadilika na kuwa 'twist'. Huu ni mtindo wa zamani miaka ya '60 uliokuwa ukipigwa na kina Jean Mwenda Bosco Losta Abelo, Daudi Kabaka, na wengineo.

**Willy Paul ft Rayvanny-Mmmh**

WILLY Paul, msanii anayekuja juu hivi sasa, mwaka huu ametoa ngoma yake iliyo kwenye mtindo wa reggae. Ngoma hiyo, anamshirikishwa msanii mwingine maarufu nchini Rayvanny. Inaitwa 'Mmmh'. Ingawa uko katika mtindo wa reggae, lakini ni wa mapenzi, maudhui ambayo ndiyo kwa asilimia kubwa yanapendwa na wasanii wa kisasa.

**Vanessa Mdee ft Gnako-Wet**


MWANADADA Vanessa Mdee naye hakuwa mbali na staili hii ya 'reggae' kwani naye alitoa ngoma aliyooiita 'Wet' akimshirikisha Gnako. Ni wimbo wa mapenzi, lakini ilionekana zaidi kuwa mtunzi alikuwa anahitaji kuchezesha zaidi mashabiki wake kuliko ujumbe. Hauna maneno mengi, zaidi ya mapigo ya staili hiyo ukichizisha mashabiki.

**Maua Sama-Let Them Know**

MAUA Sama naye hakuwa nyuma, yeye ana ngoma yake aliyoiimba kwa lugha ya Kingereza na Kiswahili kwa mtindo wa 'reggae'.

Ni wimbo wa mapenzi unaitwa 'Let Them Know' ukiwa na maana kuwa 'waache wajue'.

Huu nao unaingia kwenye orodha ya baadhi ya nyimbo za wasanii wa Kitanzania walioimba wa staili ya 'reggae', mtindo uliokuwa unatumiwa na hayati Bob Marley.



# Vijimambo

1. Hii ndio inaitwa 'nikinywa maji, nakuona kwenye glasi' - Agatha Mbale, Moro Town.
2. Ai weeewe, naoomba - Ebby Mbwambo, Tanga.
3. Hahahaaa, endelea kuomba tu mzee baba, atakupa tu - Maunda Alawi,
4. Duuh, kweli utoto kazi! Kidume kinategemea kabisa kimegewe mkate! - Beneali Moussa, Zenji.
5. Naomba, ukinipa na mie nikinunuliwa soda nakupa - Mauwa Minde, Kibada Kigamboni DSM.
6. Lazima huyo dogo atakua wa Bush Stars, anaiomba picha mkate! - Sultani Ubwa, Kibada DSM.
7. Endelea tu kuomba, huyo siyo mchoyo atakumegea tu - Moussa Beneali, Migombani Zenji.
8. Kama ulikuwa hujui tafsiri halisi ya neno 'zwazwa', basi ndio hiyo - Beneali Moussa, Migombani Zenji.
9. Naenda kukusemea kwa mama yako umeomba mkate kwa watu ->Julius Anthony, Usagara Tanga.
10. Acha uchoyo wewe, mwenzio anakuomba ndio unaingiza wote mdomo! - Mama Nah, Manzese DSM.
11. Mwache na uchoyo wake, na wewe ukinunua vitu vyako usimpe - Rehema Bwahoja, Buguruni DSM.
12. Dogo utachubuka 'makongoro' kwa kupiga magoti, hiyo picha tuu - Subira Bwahoja, DSM.
13. Jamani, si mngemuambia kama hiyo ni picha tu sio mtu kweli. Ona sasa anavyotia huruma - Dule DSM.
14. Yes, hiyo ndio dawa ya ombaomba. Kesho leteni roli lenye picha ya hela - Kijusi, Magomeni Mapipa DSM.
15. Daaah, mjukuu wa 'Matonya' anadhalilika hivi hivi kwa picha tu - Kijusi, Magomeni Mapipa DSM.
16. Huyo naye kubwa zima hajajua tu picha na mtu wa ukweli? Muacha achune magoti - Kole, Msata Pwani.
17. Hapo atalifuata gari mpaka wapi kwa kupiga magoti hivyo Magdalena Kachenja, Mabwepande DSM.
18. Tatizo dogo hajafunguka, anataka mkate au anataka uchumba - Alli Shaaban Mpanjira, Mbagala Kuu DSM.
19. Kweli walimu wanakazi. Huyo mpaka aje kujua hiyo ni picha tu si atakua Chuo Kikuu! - Pili Mpanjira DSM.
20. Mmmh, mie mgeni hapa, acha nipite tu! - Abass Ngulunga, Msasani Macho, DSM.
21. We mtoto utagongwa na magari buree. Huyo sio mtu kweli ni picha tu - Bernad Isuja, Makore Dodoma.


**SMS Bomba ya Leo:**

**Tatizo dogo hajafunguka, anataka mkate au anataka uchumba -Alli Shaaban Mpanjira, Mbagala Kuu DSM.**

## PICHA MPYA



**TUMA MESEJI - 0773 477311**




# siyo libwata, mngeuliza kwanza

**Na Adam Fungamwango**

DHANA, hisia na maamuzi ya haraka ni kitu kibaya. Binadamu anatakiwa kuwa na muda wa kutafakari chochote anachoona, kuambiwa au kusikia kabla ya kutoa maamuzi.

Haraka yoyote inaweza kufanya kutoa maamuzi ambayo siyo na baadaye kujuta.

Jamaa mmoja alikuwa anaendesha gari akielekea mjini, anakutana na mwenzake aliyekuwa akitoka mjini kwenda nje ya mji. Yule aliyetoka mjini akashusha kioo na kumwambia mwenzake 'pundaa'.

Kwa haraka, mwenzake anajua amemtukana, anamjibu 'punda mwenyewee'.

Kwa hasira akaongeza spidi ya gari na mita kadhaa baadaye akakutana na kundi la punda barabarani, hakuwa na uwezo wa kufunga breki ghafla akawaparamia na kupata ajali mbaya.

Akiwa hospitali alimkumbuka yule jamaa na kugundua hakuwa anamtukana ila alimtaarifu kuwa mbele kuna punda. Kuna mifano mingi juu ya hili.

Kwenye mapenzi nako, kuna watu wanaodhani kuwa baadhi ya wanaume wamepewa limbwata na wake zao, hivyo wanatawaliwa.

Hii iko kwenye filamu iitwayo 'Hiyari Yangu', iliyochezwa na wasanii wengi, lakini maarufu ni Simon Mwapagata, Suleiman Barafu, Wellu Sengo, Muhogo Mchungu na wengineo.

Mwapagata na mkewe Wellu wanaonekana kuishi maisha ambayo ni tofauti na ilivyozoeleka.

Mume anapika chakula, anafua nguo na kufanya kazi zote za ndani, huku mkewe akiwa ametulia tuli.

Hali hiyo inamkera mno kaka wa Mwapagata, aitwaye Barafu ambaye anamkanya ndugu yake asiwe bwege. Hata hivyo yote hayo hayakusaidia, jamaa aliendelea na kazi zote za nyumbani, huku mke akiwa na kazi ya kupeleka watoto shule na kuwarudisha, lakini anaporejea anatulia tu nyumbani huku akichati na simu.

Hali ilipozidi kuwa mbaya, Barafu akaamua kuondoka nyumbani kwa mdogo wake kwani hakuweza kuvumilia hali ile. Akakimbilia kwa baba yake mdogo, Muhogo Mchungu na kumweleza kuwa mdogo wake amepewa limbwata na mkewe, kwani imefikia wakati sasa anakuna hadi nazi, mkewe akiwa amekaa tu.

Muhogo naamua kufunga safari hadi kwa mtoto wa ndugu yake na kukuta yale yale aliyosimuliwa.

Pamoja na kumuweka chini mkewe akiwa hayupo, lakini Mwapagata hakusikia, aliendelea na kazi zake kama mtoto wa kike.

Alipoondoka wenyewe walicheka na kukumbushana kuwa bado siku tatu tu.

Wellu, mke wa Mwapagata anaitisha kikao cha wanandugu wote, lakini wa kiume baadhi walisusa, kutokana na walichokiona. Kwenye kikao hicho Wellu alifafanua kuwa mumewe aliamua kufanya kazi zile kwa hiari yake kwa muda wa mwezi mmoja ambao yuko likizo ili kuangalia uzito na kazi za kinamama.

Akasema walikuwa wanabishana na mumewe kwa kuwa kuna wakati mke analalamika kuwa anachoka, hivyo akasema atakapopata likizo atakuwa akifanya kazi zote za ndani ili aone kama zinachokesha kweli au la.

Mwapagata alikiri hilo na kusema kuwa kesho akianza kazi ofisini na kazi za ndani zitaendelea kwa mkewe kama kawaida na hali ile haikuwa kama wengi walivyotafsiri kuwa amelishwa limbwata. Wengi walishangaa na wambea wakabaki midomo wazi.




# IMEMNOGEA

## NICKI MINAJ ANAPOLEWA PENZI LA UTOTONI

RAPA mwenye vituko vingi Marekani, Nicki Minaj, hatimaye ametangaza ndoa na rafiki yake wa utotoni Kenneth Petty.

Tamko hilo ambalo limewashtua watu wengi ambao wanamfahamu mwanamuziki huyo, amelitoa baada ya kuchukua leseni ya ndoa mapema wiki hii.

Imeelezwa Mick Minaj na Kenneth wamekuwa wapenzi tangu miezi saba iliyopita, kabla ya kuamua kuweka wazi uhusiano wao kupitia ukarasa wa Instagram.

Micki alikuwa akizungumzia uamuzi wake huo kwa mwanaume huyo ambaye alimwita mume wake katika kipindi kimoja cha asubuhi kinachorushwa na redio moja ya nchini humo.

"Tumeshapata leseni ya ndoa, nafikiri nilimtafuta kabla, sasa nina furaha," alisema.

'Ilikuwa vigumu kupata furaha, sasa nipo huko siwezi kumhakikishia kila mtu kwa kila kitu," aliongeza mwanamuziki huyo.

Nicki amewaeleza marafiki zake kwamba 'mume wake' huyo Kenneth anampa mapenzi motomoto kila siku jioni kila anapotoka kuoga. Hata hivyo amekiri kuwa bado ndoa hiyo haijakuwa rasmi.

'Kila usiku pale ninapotoka kuoga mume wangu anachukua mafuta ya kurainisha ngozi na kunifanyia 'miguuni', mapajani na sehemu ambayo muhimu ambayo mtu mwingine hawezi kugusa," alisema na kuongeza "...Ni mahaba tu,'

Rafiki wa Nicki hivi karibuni alimsifu Kenneth kwa kumfanya ajisikie mwenye nguvu.

"Yuko katika hali bora amekuwa naye kwa muda mrefu kiroho".

Kauli hiyo inaungwa mkono na mwanamuziki huyo akisema "Ikiwa mimi ni mwaminifu kiroho, niko mahali bora zaidi kuliko nilipokuwa kwa muda mrefu".

Amesema mume wake anamjua kihalisia na hawawezi kuigiza kwani wamekuwa karibu miaka mingi hali ambayo hawawezi kuchokana.

Mrembo huyo mzaliwa wa Trinidad ni rapa wa mwanamke aliyepewa tuzo nyingi nchini Marekani.

Mwaka 2015 alishinda tuzo ya kuwa mwimbaji bora wa Hip-Hop katika singo yake ya "Anaconda".

Alishinda tuzo ya BET kama Msanii Bora wa Kike katika muziki wa hip hop mwaka 2010 na 2016.

Mwaka 2011 hadi 2016, Minaj alichaguliwa kwa jumla ya tuzo 10 za Grammy.

# Burna Boy na mama yake mmh!

VIDEO ya mama wa mwanamuziki nyota, Burna Boy na mtoto wake huyo, imezidi kugusa hisia za watu wengi na kusababisha kugeuka kuwa filamu tamu.

Mwanamuziki huyo na mama yake walitupia video fupi wakionekana wakiserebuka juu ya jukwaa baada ya nyota huyo wa muziki nchini Nigeria kushinda tuzo maarufu za BET.

Baadhi ya mashabiki walionekana kufurahia jambo hilo na kupendekeza video hiyo kuchaguliwa kuwa ya mwaka katika nchi hiyo.






## Tonto apasua jipu la zilipendwa wake

SIKU chache baada ya mume wake kumtambulisha mpenzi wake mpya, mwigizaji kutoka Nollywood, Tonto Dikeh, ametoa siri kwamba alikuwa akipigwa kila mara na mwanaume huyo.

Tonto alitoboa siri hiyo baada ya kushiriki katika mjadala uliokuwa ukizungumzia namna wanaume wanavyowanyanyasa wake au marafiki wao wa kike kwa kuwapa vipigo.

Katika mjadala huo ndipo alipobainisha kwamba mume wake wa zamani Olakunle Churchill alikuwa akimpiga kila mara.

## Upoo?...Davido anakuita

BAADA ya siku kadhaa kusambaa kwa video ya mwanamke mmoja akililia kuonana na supastaa wa muziki wa Nigeria, Davido, mambo yameanza kumnokea ghafla.

Mwanamuziki huyo amejibu maombi hayo na kueleza yupo tayari kuonana na mwanamke huyo na kuwaomba mashabiki wake kuhudhuria katika tukio hilo.

Davido aliposti katika akaunti yake ya Instagram akisema anamtafuta mama huyo na kueleza ana uhakika mambo yatakuwa sawa pale atakapoona ujumbe huo.





## We Venita umekula nyama, mkia unakushindaje?

Venita Akpofure ameungana na wasanii maarufu waliojikuta wakivunja uhusiano wao kimapenzi na wenza wao mwaka 2019.

Mrembo huyo ambaye ni maarufu nchini humo ameamua kuachana na mpenzi wake huyo baada ya kuwa katika uchumba kwa muda wa miaka minne.

Akitumia akaunti yake ya Instagram, alimwandika ujumbe akisema ameamua kuchukua hatua hiyo baada ya kuchoshwa na vitendo vya unyanyasaji vinavyofanyika.

## Hongera Omotola, ukisikia ulezi ndiyo huo

MWIGIZAJI mkongwe Omotola Jalade-Ekiende, amekuwa na furaha baada ya binti yake wa pili Meraiah, kupata digrii ya pili akiwa na umri wa miaka 19 pekee.

Omotola amekuwa mwanamke mwenye furaha aliposhuhudia mtoto wake huyo akivishwa joho na kuashiria amehitimu elimu hiyo katika chuo kikuu nchini Cyprus.

Katika ukurasa wake wa Instagram, msanii huyo anayezeeka na urembo wake alisema anaona fahari kuwa karibu na mwanawe huyo ambaye anamfananisha na pacha wake.



SAFU



## Mionzi ya Sheria

Na John Juma
0716217615

# Ulinzi wa kisheria kwa wajane

KUTOKANA na maadhimisho ya Siku ya Wajane Duniani, ambayo hufanywa Juni 23 kila mwaka, ni vema kujifunza zaidi kuhusu haki za wanawake hawa waliofiwa na wenza.

Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971, Sura ya 29 iliyorekebishwa mwaka 2010; sanjari na Sheria ya Usimamizi na Uendeshaji wa Mirathi Tanzania Sura ya 352, marejeo ya mwisho 2002, zinaainisha haki hizo.

Kwa ujumla ziko aina mbili za mali anazostahili mke wa marehemu au mjane.

Mosi, ni mali inayotokana na mali za walizochuma pamoja na mumewe wakati wa uhai wake.

Pili ni urithi anaostashili kupata kama mrithi halali wa marehemu mumewe.

Vifungu vya 2(1); 60 (b); na 114(1)-(3) vya Sheria ya Ndoa Sura ya 29 ya mwaka 1971 iliyorekebishwa mwaka 2010.

Kwa mfano, mume amefariki. Lakini kabla hajafa walijenga nyumba pamoja na mkewe. Au walinunua kiwanja au gari. Mume baada ya kufariki ameacha mali hizo.

Isitoshe pia, kwa kufuatia msingi huo huo, katika mali husika kuna "share" ya mume, kadhalika ya mke. Na zaidi sana, "share" ya kila mmoja inatokana na ukweli kuwa kila mwanandoa, wote kwa pamoja wamechangia nguvu katika kufanikisha kupatikana kwa mali hizo.

Shauri maarufu la Hawa Mohamed dhidi ya Ally Seif [1983] kwa kuzingatia uamuzi wa kimahakama uliofikiwa kupitia shauri hilo, itoshe kuongeza kwamba mchango huo siyo tu ule wa leta ni lete, kwani hata kazi za nyumbani zinazofanywa na mke au mume kama kupika, kufua, kulea watoto ni mchango katika kupatikana kwa mali hizo.

Lakini, pia bado ni muhimu kwa wanandoa kufahamu na kuzingatia kwamba "mchango hasi"; kama vile matumizi mabaya ya fedha na rasilimali za familia vinaweza siyo tu kumpunguzia mhusika sehemu ya haki ya gawio, bali hata kumkosesha kabisa.

Tatu, endapo mume amekufa, mwanamke anastahili urithi kutoka mali za marehemu mumewe. Urithi huo utatokana na mali zilizokuwa zikimilikiwa na mume na yeye pia.

Jambo hili ni kusema kwamba urithi huo utatokana na "share" au sehemu ya mali ya mume na siyo ile ya mke, ambayo tayari ni stahiki yake.

Tena, mjane anazo tena atakuwa na haki za aina mbili ya kupata sehemu yake aliyochangia katika kupatikana kwa mali husika, sambamba na haki ya kurithi mali ya marehemu mumewe.

Taratibu za Kufuata

Kinachotakiwa kufanyika, awali ya yote, ni kutambuliwa kwanza sehemu ya mali ambayo ni sehemu ya mchango wa mke katika kupatikana kwa mali husika na kutengwa na kuwekwa pembeni.

Mfano kama ni nyumba ya vyumba sita na pengine mchango wa pamoja wa mke na mume ni nusu kwa nusu, bilashaka vyumba vitatu vitawekwa pembeni kama sehemu ya mchango wa mke huyo na vile vyumba vitatu ambavyo vitabakia ndiyo vitatakiwa kugawanywa kama urithi halali kwa kuwa warithi (wote) watakakuwepo.

Itajumuisha mke wa marehemu (mjane) na watoto kama wapo. Ile hoja eti kuwa alishapatiwa vyumba vitatu hapo mwanzo haitakuwa na msingi.

Ieleweke kuwa urithi siyo jasho la nguvu kazi au rasilimali za mhusika, bali hutokana na mapenzi ya mtoa wosia na matakwa ya lazima ya kisheria kwa maslahi ya wanufaika ambao ni lazima kupata stahiki zao akiwemo na mke wa marehemu .

Kufuatilia Mahakamani

Katika mazingira hayo kukusudia ni muhimu kwanza kwa msimamizi wa mirathi au wasii kuthibitishwa au kuidhinishwa na Mahakama.

Ambapo basi, anaweza kuwa alishateuliwa au kutajwa na marehemu katika wosia au kama hakuna wosia atateuliwa na kupendekezwa na ndugu kwenye kikao cha familia.

Vifungu 2(1); 3; 9; 16(a)-(d); na 17 vya Sheria ya Usimamizi na Uendeshaji wa Mirathi Sura ya 352 vinaeleza.

Baada ya mahakama kumthibitisha msimamizi wa mirathi au wasii, kwa mujibu wa taratibu, mjane ataweza kudai haki yake ya kwanza inayojumuisha mali walizochuma pamoja na mumewe.

Katika mali zilizoachwa na marehemu, kabla ya mgao wa mirathi kuanza kuchukua hatamu kwa kuzingatia haki za warithi wengine na haki hii ataidai kwa msimamizi wa mirathi.

Na kama mjane ndiye msimamizi wa mirathi basi haki hii ya mali walizochuma pamoja ataidai kwa warithi.

Kwa lugha nyepesi zaidi, atapata sehemu yake baadaye urithi. Na mwisho, kama kutakuwa na mgogoro au ubishi, utata mjane huyo ili kulinda maslahi yake, atatakiwa kufungua Shauri la Malalamiko Mahakamani na kuiomba itoe tamko kuhusu hatima ya kupata sehemu au share yake katika mali zilizochmwa pamoja na mumewe.



## Kalamu ya Mwalimu

Reubeni Lumbagala

# Wananchi mhimili ujenzi miundombinu ya elimu-3

KARIBU msomaji wa safu hii ya "Kalamu ya Mwalimu" katika mwendelezo wetu wa makala hii hii yenye kichwa "Wananchi nguzo muhimu ujenzi wa miundombinu ya elimu - sehemu ya tatu. Katika kazi zilizotangulia nilieleza namna wananchi wa Wilaya ya Kongwa walivyojitolea nguvukazi ili kusimamisha maboma na hatimaye serikali na ofisi ya mbunge kuunga mkono jitihada za wananchi hao kwa kutoa fedha na vifaa vya ujenzi ili kukamilisha madarasa katika shule mbalimbali za msingi na sekondari wilayani humo.

Leo niendelee kuangazia wananchi wa maeneo mbalimbali walivyoshiriki katika shughuli za maendeleo hasa katika sekta ya elimu kwa kuhakikisha madarasa, vyoo na ofisi vinajengwa ili wanafunzi waweze kusoma katika mazingira bora na hatimaye kupata elimu bora kwa maendeleo endelevu.

Wananchi wa mkoani Simiyu hawajabaki nyuma. Katika kuhakikisha wanatoa nguvu kazi na michango yao na hali na mali ili kukamilisha majengo na hatimaye serikali kuwapatia fedha za kukamilisha maboma hayo ili yawe madarasa bora na ya kisasa kwa ajili ya kutolea elimu bora kwa wanafunzi.

Wana Halmashauri ya Mji wa Bariadi wamejitolea nguvukazi kwa kuchimba msingi wa ujenzi wa vyumba vya madarasa zaidi ya 40 na mabweni 15 kwa ajili ya Shule ya Sekondari Simiyu.

Kukamilika kwa miundombinu hiyo, kutasaidia shule hiyo kuwa na uwezo wa kudahili wanafunzi wengi zaidi.

Huko mkoani Ruvuma, wananchi wanashiriki kazi za ujenzi wa madarasa ili watoto wao waweze kusoma katika mazingira bora yanayovutia ufundishaji na ujifunzaji wenye tija.

Katika Wilaya ya Namtumbo mkoani Ruvuma, kwa juhudi za Mkuu wa Wilaya hiyo Sophia Kizigo, wananchi wa kata ya Mgombasi wamekubali kujenga madarasa mawili hadi kufikia maboma, kisha serikali kumalizia palipobakia ili kusaidia wanafunzi wa chekechea na darasa la kwanza kujifunza katika mazingira mazuri.

Wananchi wa Kata ya Rasibula katika Halmashauri ya Manispaa ya Lindi waliamua kujenga shule ya sekondari katika mtaa wa Mitwero ili kuwaondolea adha wanafunzi ya kutembea umbali mrefu kupata elimu ambayo ni hali yao ya msingi.

Hii inaonyesha mwamko mkubwa walionao wananchi katika kuiunga mkono serikali katika jitihada za kuboresha mazingira ya utoaji wa elimu bora.

Aidha, wilayani Hai mkoani Kilimanjaro, wananchi wa Kijiji cha Kwa Sadala, waliunga mkono juhudi za serikali za kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia shuleni ambapo walifanikisha upatikanaji wa madarasa matatu katika Shule ya Msingi Msamadi kwa kutoa nguvukazi na michango yao.

Juhudi hizi zimewezesha wanafunzi kusoma katika mazingira bora kwa kuwa na madarasa mazuri na ya kisasa.

Pongezi kwa wachimbaji wadogo wa madini ya dhahabu wa Kata Nyaruguru wilayani Geita mkoani Geita, ambao walijitolea kuchangia ujenzi wa madarasa manne na ofisi mbili za walimu kwenye Shule ya Msingi Tologo iliyogharimu Sh. milioni 56.

Wachimbaji wadogo walifikia uamuzi huu baada ya upepo mkali kuleta uharibifu katika madarasa ya shule hiyo. Uamuzi wa wachimbaji wadogo wa kukarabati shule hiyo umesaidia wanafunzi hao kuendelea kupata haki yao ya msingi ya kusoma na kufikia elimu bora.

Desemba 2017, Mkuu wa Wilaya ya Gairo mkoani Morogoro, Sirieli Mchembe, alitoa taarifa ya mapato yatokanayo ya michango ya wananchi wa kata ya Chakwale, kwamba ndani ya miezi mitatu, wananchi hao walichangia milioni 33 kusaidia sekta ya elimu.

Mchembe aliendelea kusisitiza kuwa "Wilaya ya Gairo ina madarasa zaidi ya 30 yote yamejengwa kwa nguvu za wananchi hadi ngazi ya boma, bado kuezekwa.

Madarasa haya ni nje ya mengine 16 yaliyomalizika ndani ya mwakammoja. Mpaka sasa hatuna darasa ya nyasi wala wanafunzi wanaokaa chini. Tumemaliza nyumba za walimu nane, maabara sita na tuna maboma yanayohitaji nguvu ya ziada."

Hakika, upo mwamko wa wananchi kujitolea nguvukazi katika ujenzi wa miundombinu ya elimu katika maeneo mbalimbali ya Tanzania.

Japo juhudi zaidi zinapaswa kufanyika ili maeneo yote wananchi wawe na mwamko wa kujitolea ili kuleta manufaa katika sekta ya elimu.

Muhimu, ni viongozi katika maeneo yao kuwa chachu ya kuhamasisha wananchi kujitolea kwa maendeleo ya elimu ambayo ni sekta nyeti kwa kwa taifa lolote.

Pia viongozi wawe mfano wa kuigwa katika kuchangia fedha na nguvukazi zao ili wananchi wajifunze kutoka kwao, kwani kuongoza ni kuonyesha njia.

Wananchi waamke, washiriki shughuli za maendeleo kwa faida ya kizazi cha sasa na kijacho. Hili likifanyika kikamilifu katika sekta ya elimu na sekta nyingine, taifa litapiga hatua kubwa kimaendeleo na kwa muda mfupi. Tafakari.

**Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilayani Kongwa mkoani Dodoma.**

**Maoni: (+255) 0764 666349**

SALAM ZA KWA HERI KUTO

# Haya ndiyo matokeo y za ushirikiano wetu In

Na Sandeep Arya

TAREHE 15 Juni 2019, nimeondoka Tanzania baada ya kupata uzoefu usio na mfano wa takriban miaka minne katika ardhi au nchi hii adhimu na isiyoweza kusahaulika.

Hii inaadhimisha mwendelezo wa hisia utokanao na maendeleo imara, yatokanayo na urafiki uliopo baina ya India na Tanzania, pamoja na mshikamano katika nyanja mbalimbali, kukubalika kwa hali ya juu na msaada kutoka kwa serikali rafiki.

Pia, hapo kuna ukarimu na upendo wa watu waliojawa na upendo mkubwa na fikra/hisia zangu kuona uhusiano na ushirikiano umeendelezwa katika miaka hii, pamoja na nchi hii iliyo katika mipaka asili ya kipekee.

Miaka yangu ya kazi hapa Tanzania, imegusa karibu maeneo yote ya kidiplomasia na ushirikiano baina ya nchi mbili hizi ambayo yana mizizi mirefu na nguvu za urafiki uliopo baina ya India na Tanzania.

Maelewano ya pamoja imara na ya kudumu na kuthaminiana baina ya serikali mbili, ambazo zimeanzishwa kutokana na misingi imara kwa lengo la maendeleo na mafanikio tangu enzi za Mwalimu Julius Nyerere, kwa madhumuni ya kuimarisha maendeleo ya kimahusiano baina ya India na Tanzania.

Ziara ya Waziri Mkuu, Narendra Modi, mwezi Julai mwaka 2016 kuja kukutana na Rais Dk. John Pombe Magufuli, palifuatiwa na kikao cha Tume ya Pamoja iliyoongozwa na wenyeviti wa pamoja wa Mawaziri wa Mambo ya Nje mwezi Oktoba 2018 na Kamati ya Pamoja ya Biashara mwezi wa Agosti 2017 na mikutano ya maofisa mbalimbali katika sekta za afya, elimu, maji, kilimo, madini na nishati.

Hivi ni vielelezo vya juhudi endelevu katika kuhusiana, kushirikiana na kuendeleza mahusiano ya pamoja baina ya serikali hizi mbili.

Upana wa ushirikiano wetu kiuchumi na biashara si wenye kuonekana kirahisi siku zote. Mwaka hadi mwaka, India imekuwa ikipokea zaidi ya asilimia 20 ya bidhaa zote za mauzo ya nje za Tanzania. Hii inatokana na mpango wa msamaha wa ushuru wa forodha/kodi uliotolewa na India kwa Tanzania takriban zaidi ya miaka 10 iliyopita.

Takwimu za TRA kwa mwaka 2018, zimeiweka India kwa mara nyingine kuwa ndiye mshirika mkuu kinara wa Tanzania kibiashara, ikiwa na takriban jumla ya Dola za kimarekani bilioni mbili, thamani ya jumla ya biashara baina ya nchi mbili hizi, kuwa katika nafasi ya tano katika miongoni mwa wawekezaji wa Tanzania.

Hilo ni jambo la kujivunia kwa India, ambayo yenyewe inavutia uwekezaji unaofikia Dola za kimarekani bilioni 40 kwa mwaka.

Kampuni kadhaa za India zimekuwa zikifuatilia fursa mpya nchini Tanzania katika maeneo mbalimbali kama vile dawa, magari, kilimo, miundombinu, uzalishaji wa bidhaa za viwandani na huduma.

Ni kasi pekee, na siyo mtiririko (trend), ndiyo jambo lenye kuleta mtazamo wa mbele katika mahusiano ya kiuchumi baina ya India, ikiwa ni nchi yenye uchumi mkubwa unaokua kwa kasi na Tanzania, ikiwa nchi yenye matumaini makubwa ya uchumi zinazokuwa barani Afrika.



Waziri Mkuu wa India, Narendra Modi (kushoto), alipozuru nchini,



Waziri Mkuu wa India, Narendra Modi (kushoto), akipungia wananchi waliojitokeza kumpokea. Kulia ni Rais John Magufuli. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

Ushirika wa kimaendeleo, ni jambo la kuvutia na lenye maendeleo ya kasi katika mahusiano yetu ambayo yanahusisha sekta za maji, afya, elimu, kilimo na maendeleo ya utaalamu.

**SEKTA YA MAJI**

Ushiriki wa India katika sekta ya maji nchini Tanzania wenye jumla ya pesa za mkopo wa masharti nafuu upatao takriban shilingi trilioni 2.4, ni jambo la faraja sana kwa India.

Mchango wa takriban asilimia 26 wa maji yote yanayosambazwa na Dawasco katika jiji la Dar es Salaam kutoka katika mradi wa awali wa maji unaogharimu takriban shilingi bilioni 320 unahudumia watu wapatao milioni moja katika Jiji la Dar es Salaam.

Mradi wa pili mkubwa wa kusambaza maji Tabora, Nzega, Igunga na vijiji vitavyopitiwa na mradi huo, ambao unagharimu zaidi ya shilingi bilioni 600; hivi sasa umekamilika kwa asilimia 70 na unapaswa kukabidhiwa mnamo mwezi Februari 2020.

Isitoshe, miradi iliyoahidiwa, ambayo ipo katika usanifu hivi sasa, itajumuisha miji 28, ikiwamo Manisipaa ya Zanzibar, hivyo basi itashuhudia mchango mkubwa sana wa India katika sekta ya maji nchini Tanzania kwa miaka mingi ijayo.

Mamia ya wahandisi wa maji nchini Tanzania wamepata mafunzo nchini India kwa ufadhili kamilifu kwa miongo kadhaa iliyopita ambapo inatoa uwezo wa kuimarisha uendelevu wa rasilimali za maji zilizopatikana.

India imejiingiza katika ujenzi wa vifaa na uwezo kwa afya, elimu, kilimo na maendeleo ya ujuzi katika sekta kama vile Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama), nishati, maendeleo vijijini, ujasiriamali, huduma za fedha na miamba.

Takriban maofisa 500 wa Kitanzania na wataalamu mbalimbali huenda India kila mwaka kwa mafunzo mbalimbali ambayo yanafadhiliwa na India. Ushirikiano wa kimaendeleo unapaswa kujikita katika mahusiano na ushirikiano wa muda mrefu baina ya nchi mbili hizi.

Ushirikiano baina ya nchi mbili hizi unagusa sekta kama vile ma-

MAKALA

## OKA KINYWANI KWA BALOZI ...

# ya juhudi endelevu ndia na Tanzania



Julai mwaka 2016, akiwa na mweyeji wake, Rais Dk. John Magufuli.

pambano dhidi ya dawa za kulevya, masuala ya bahari, mafunzo ya ulinzi, ikijumuisha ulinzi wa amani wa Umoja wa Mataifa, matumizi ya kijamii ya utaalam wa nguvu za mionzi, na maeneo kadhaa muhimu ya kitaalamu yenye maslahi ya pamoja.

Serikali zetu zimekuwa zikijadiliana kila mara na kugundua maeneo ya msingi kwa Tanzania, ili kuendeleza ushirikiano wetu. Nishati ya jua na mengineyo kama vile pampu za jua na taa kupitia mpango wa Jumuiya ya Kimataifa ya Nishati ya Jua (International Solar Alliance) iliyoanzishwa na India kwa kushirikiana na Ufaransa, pamoja na Tanzania ikiwa mwanachama, inatoa fursa kubwa na nyingi katika miaka ijayo.

Sababu kuu za urafiki baina ya India na Tanzania ni mshikamano, upendo na maelewano ya watu wa nchi mbili hizi, ambayo vipo baina yao. Hiyo inawezekana kutokana na kufanana kwao katika safari za mendeleo yao ya nchi mbili hizi, urafiki ikiwa sehemu ya tabia za watu wa nchi mbili, matarajio ya jamii zetu kwa ajili ya maendeleo na mafanikio au uhusiano ya kina wa kihistoria baina ya watu wa nchi mbili hizi na katika maingiliano yao.

Jamii ya Watanzania wenye asili ya India inaakisi asili ya kihistoria ya muunganiko baina yetu. Kilicho dhahiri ni kwamba watu nchini India na Tanzania wameungana pasipo mfano. Kuna ushirikiano wa kitamaduni na kutembeleana kati yetu ni kielelezo tosha kinachoonyesha mshikamano wetu.

Safari za moja kwa moja za Shirika la Ndege la Tanzania (Air Tanzania), kutoka Dar es Salaam hadi Mumbai mwezi ujao, ikiwa kituo cha kwanza nje ya Afrika, itaimarisha na kusaidia mno mahusiano haya baina ya nchi mbili.

Natoa shukrani za dhati kwa serikali na watu wa Tanzania kwa ukarimu wao na msaada wao kwangu kwa kipindi chote cha miaka minne. Hii ilinitia nguvu kubwa na motisha wa kufanya kazi ya kukuza uhusiano baina ya India na Tanzania katika sekta mbalimbali.


Nimeshawishika kwamba uhusiano huu una hatima nzuri katika siku za baadae, katika msingi imara na muunganiko madhubuti baina yetu. Nitathamini na kuenzi kwa kiwango cha hali ya juu kumbukumbu adhimu za nchi hii ya kipekee "isiyoweza kusahaulika", kwa watu wema na wakarimu, upendo wao na mitazamo yao chanya kwa nchi ya India na ushirikiano wangu wa karibu na serikali na watu wa hapa.



Balozi Sandeep Arya, katika majukumu yake nchini, katika miaka minne aliyoishi nchini.

**• Sandeep Arya, alikuwa Balozi wa India nchini Tanzania na Mwakilishi wa India katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, tangu Agosti 2015 hadi Juni 2019)**

## CHEMSHABONGO NA NIPASHE NAMBA (00 7 00)




**Dondoo: Kulia**

1. Nchi yenye miji mikuu mitatu
8. Mzazi wa kiume 9. Upesi
10.Mfalme wa pili wa Israeli
11.tia hatiani
12.Jina la zamani la Malawi
15.Chanzo 16.Dalili ya kitu
18.Taka kwa unyenyekevu
20.Mji mkuu wa Somalia
22.Uvunjaji ungo
24.Ndege asiyeruka
25.Sema hapana
27.kaka wa mama
28.kitu au jambo linaloashiria

**Dondoo: Chini**

1. Watu wa Ghana
2. Chana vipande
3. Kuongezeka kimo
4. Ukweli wa jambo 5. fichua
6. toa tangazo kwa sauti kubwa 7. Shetani
13.Furaha
14.Bandari kubwa Angola
15.Mzungu wa Afrika ya kusini
17.Mpiganaji wa Kijapani
18.Safisha kwa maji na sabuni
19.mtu wa asili ya Bara Hindi
21.Starehe 23. dumu
26.Kagua

## Jibu Na: 6



# Shule zifundishe athari, kukabiliana na tabianchi

Na Jennifer Julius

MABADILIKO ya tabianchi ni janga linaloumiza vichwa mataifa mbalimbali hasa ukizingatia kuwa athari zake sasa zinaonekana bayana.

Ripoti ya tathmini ya mabadiliko ya tabianchi iliyotolewa na jopo la kiserikali la kimataifa, linalofanya kazi ya kutathmini mabadiliko ya hali ya hewa kidunia (IPCC), inasema kuwa kama jitihada zisipofanyika, kufikia mwaka 2030 joto la dunia litaongezeka kufikia nyuzi joto 1.5.

Na hali ikiendelea kuwa hivi, mpaka kufikia mwaka 2052 nyuzi joto zitapanda hadi 2.0 hali ambayo ni hatari kwa viumbe hai wa baharini.

Taarifa za mazingira za Umoja wa Mataifa zinazozungumzia ongezeko la kiwango cha kina cha maji baharini, zinasema kuwa viwango vya maji ya baharini kote duniani vimekuwa vikiongezeka karne moja hadi nyingine.

Lakini katika miaka ya hivi karibuni takribani muongo mmoja uliopita kasi ya ongezeko hili imezidi kuwa kubwa na kwamba mwaka wa 2017 bahari iliongezeka kwa inchi tatu, hii ikiwa ni zaidi ya kiwango cha wastani kilichotabiriwa mwaka 1993.

Ni wazi ongezeko la joto duniani linaathiri nchi kavu na bahari, hii inamaanisha kuwa kuna kupanda zaidi kwa kina cha bahari. Hivyo bila kuhakikisha matumizi na ulinzi endelevu wa bahari ni wazi eneo hilo litakuwa limeathiriwa zaidi na mabadiliko ya tabianchi.

Kuna hatari kuwa baadhi ya visiwa ndani ya bahari ikiwamo Zanzibar vinatishiwa kuzama kutokana na ongezeko la kina cha maji. Kina hiki kinaongezeka kwa sababu ya kuyeyuka kwa mabonge ya barafu kwenye vizio vya dunia.

Hili si jambo la kukaa kimya ni lazima kuchukua hatua. Mwaka 2015 baadhi ya wakazi wa Mji Mkongwe walishuhudia samaki wakitapakaa barabarani baada ya kina cha bahari kuongezeka kisiwani Zanzibar.

Suala la uharibifu wa mazingira unaochangia mabadiliko ya tabianchi ni lazima kudhibitiwa kwa kuwa viumbe walioko baharini wanapoathirika na kutoweka ni wazi kuwa hata wanadamu wanakabiliwa na kitisho cha kuangamizwa pia.

Mataifa yamekutana katika mji wa Bonn nchini Ujerumani kunoa vichwa kujadili jinsi ya kufanya ili kufanikisha utekelezaji wa mikakati ya kupunguza ongezeko la joto duniani.

Mkakati ukiwekwa kuainisha namna ya kuzisaidia nchi zinazoendelea kuzuia athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mojawapo ya hoja zilizojadiliwa na ile ya kuwekeza kwenye uhamasishaji na kutoa elimu kwa umma kuhusu mabadiliko ya tabia nchi kuanzia ngazi ya elimu ya msingi hadi vyuo vikuu.

Malengo makubwa yaliyopo katika hoja hii ni kwamba ni lazima kuwajengea uwezo vijana ambao ndiyo watekelezaji wakuu wa sera hiyo na kuwawezesha kujua mabadiliko ya tabianchi ni nini na jinsi nchi zinazoendelea kama Tanzania zinavyoathirika.

Yote haya ili kuwe na vizazi vinavyojua nini kinachoendelea katika ulimwengu wanaoishi kuanzia angani kwenye jua, ndani ya utando wa ozone, baharini na kwenye vijiji na miji wanayoishi.

Mathalani Tanzania, asilimia kubwa ya vijana nchini hawana uelewa juu ya mabadiliko ya tabianchi wala hawafahamu jinsi nchi inavyoathirika kutokana na ama ongezeko kubwa la joto duniani. Vijana wengi hawaelewi kwamba nchi yao ni mwathiriki wa mabadiliko ya tabianchi yaliyosababishwa na mataifa makubwa ambayo yamechangia kumomonyoa tabaka la utando wa ozoni na kuongeza joto ulimwenguni.

Katika kuwapa elimu hiyo, kinachotakiwa kufanyika ni kujikinga na athari hizo kama vile kupanda miti ya kutosha ili kuzalisha hewa ya okisjeni kwa wingi itakayosafisha hewa na kuongeza unafuu.

Ukimuuliza kijana ni kwa nini misimu ya mvua imebadilika nan chi inapata mvua zisizotabirika? Huenda hatokuwa na jibu wala maelezo, yote ni kutokana na kwamba hawana uelewa wa kutosha juu ya jambo hlo.

Ni wakati sasa serikali na wadau kushirikiana kuongeza kipengele cha kufundisha sayansi au elimu hii kwa watoto na vijana iwe shuleni ama ndani ya jamii ili wanapokuwa wawe mabalozi wazuri wa kupambana na athari za mabadiliko hayo nchini katika kipengele cha kupunguza joto la kimataifa na kujilinda.

Sasa hivi kumkalisha mtu mzima na kumueleza athari za mabadiliko ya tabia nchi na jinsi ya kujikinga ni kwa hakika atakusikiliza lakini utekelezaji utakuwa mdogo kwa sababu ya mitizamo na fikra zake.

Ndiyo maana ni muhimu kuwapa vijana taarifa za kina vyuoni na shuleni ili wawe na elimu kuanzi elimu ya msingi hadi ngazi za juu kwenye vyuo vikuu.

Janga la athari za mabadiliko ya tabianchi linaathiri kila sekta si kwa Tanzania pekee bali ni kila taifa ndiyo maana ni wakati wa kuchukua hatua sasa na wala si kusubiri hadi kesho ili kuzuia uwezekano wa kuathirika zaidi.

Kwa hali inavyoonyesha hakuna muda wa kusubiri, ni wakati wa kufanya utekelezaji na uwe wa haraka kwa maana adui mkubwa anayeumiza katika suala hili ni kukosa elimu juu ya nini hasa kinachoendelea.

Elimu hii ikitolewa hata shughuli zinazopelekea kuongezeka kwa athari za mabadiliko ya tabianchi kama vile kukata miti ovyo zitakwisha kwa sababu asilimia kubwa ya wakataji wa miti ni vijana, hufanya hivyo kwa sababu mbalimbali ikiwemo biashara, kilimo, ujenzi na uwekezaji lakini bila kujua kuwa waingiza nchi yao kwenye matatizo.

Ndiyo serikali na taasisi zisizo za kiserikali pamoja na wadau wengine ni wakati wa kuanza utekelezaji wa maagizo ya Makubaliano ya Paris ya kuwekeza kwenye elimu ili kufikia mwaka 2030 kuwe na uhakika kuwa kiwango cha nyuzi joto 1.5 hakifikiwi ili kulinda watu, bahari na mazingira kwa ujumla.



Shughuli za uvuvi nazo zimo hatarini visiwani hapo kama hakutakuwa na mikakati ya kunusuru kisiwa kisizame. **PICHA: MTANDAO.**



Samaki wa kijani wanaopatikana kisiwani Mafia ni moja ya viumbe bahari walio katika hatari ya kutoweka iwapo kina cha bahari kitaongezeka na kisiwa hicho kuzama.

# Mbunge Jaguar akosa dhamana

**NAIROBI, Kenya**

MBUNGE wa Kenya Charles Njagua Kanyi maarufu Jaguar, ataendelea kubakia rumande kwenye kituo cha polisi kwa siku nyingine nne baada ya mahakama kumnyima dhamana.

Jaguar alikamatwa nje ya Bunge la Kenya Jumatano wiki hii na kufikishwa mahakamani juzi kujibu mashtaka ya kutoa kauli za chuki.

Mahakama imewapa polisi siku tatu zaidi kuendelea na uchunguzi dhidi ya kauli za kichochezi dhidi ya wafanyabiashara wa kigeni katika soko kuu la Gikomba nchini Kenya, zilizotolewa na mbunge huyo.

Njagua alitoa maneno makali alipokuwa akizungumza kuhusu kuwapo kwa ushindani wa kibiashara na wageni usio na usawa, alisema: "Wakenya ni sharti wafanye biashara zao bila kushindana na watu kutoka mataifa mengine. Raia wa China wametawala biashara za kuuza magari nchini humu, Watanzania na Waganda wanatawala katika masoko yetu. Tunasema imetosha iwapo hawatarajeshwa nyumbani katika saa 24 tutawashika na kuwapiga na hatuogopi mtu yeyote," alinukuliwa akisema.

Kauli hiyo iliibua hisia kali kwenye mitandao ya kijamii. Hisia hizo tofauti zilifuatia matamshi aliyotoa mbunge wa Kenya dhidi ya wafanyabiashara wa kigeni wanaoendehsa biashara nchini humo.

Katika kanda ya video iliyosambazwa nchini Kenya na katika mataifa jirani ikiwamo Tanzania, mbunge huyo mjasiriamali na mwanamuziki, alisema hawatokubali watu wa nje waje kuendesha biashara nchini.

"...Ukiangalia masoko yetu, Watanzania na Waganda wamechukua biashara zetu, sasa sisi tumesema enough is enough".

Mbunge huyo hata hivyo alisema kuwa kauli yake "ilitafsiriwa" visivyo. ***BBC***



Rais wa China Xi Jinping (kushoto) na Waziri Mkuu wa Japan Shinzo Abe, wakielekea kwenye mkutano wa G 20. **PICHA:DW.**

# Mkutano wa G20 waanza Japan

**OSAKA, Japan**

MKUTANO wa mataifa matajiri duniani yenye nguvu kubwa za kiuchumi maarufu kama G20 umeanza jana nchini Japan.

Miongoni mwa masuala tete yanayotarajiwa kuugubika mkutano huo wa kilele ni mzozo wa kibiashara kati ya Marekani na China, mvutano kati ya Iran na Marekani kuhusu nyuklia, mashambuzi ya Ghuba na mada kuhusu mabadiliko ya tabianchi.

Viongozi wa nchi 20 zenye nguvu zaidi duniani wanakutana nchini Japan kwa siku mbili.

Kikao hicho cha vigogo wa mataifa 20 wenye nguvu zaidi duniani kinafanyika katika mji wa Osaka Japan.

Mkutano kati ya Rais Donald Trump wa Marekani na Rais wa China Xi Jinping, ni miongoni mwa mikutano inayosubiriwa kwa hamu kubwa pembezoni au kando ya mkutano huo wa kilele.

Trump na Jinping wanatarajiwa kukutana leo Jumamosi.

Nchi hizo mbili zimeingia katika mvutano mbaya wa kibiashara na viongozi wengi wanasubiri kuona ikiwa viongozi hao wataweza kupata suluhisho la kumaliza uhasama huo.

Rais Trump pia alikutana na Rais wa Urusi Vladimir Putin na akamwambia huku akitabasamu tena kwa njia ya utani kuwa asiingilie kati uchaguzi wa Marekani.

Mabadiliko ya tabianchi ni miongoni mwa mada tete zinazotarajiwa kujadiliwa. Pia, Ufaransa ilisema inataka wanachama wa G20 wajitolee kuhakikisha viwango vya utoaji wa gesi chafu vinapungua na hilo liwe miongoni mwa maazimio ya pamoja ya mkutano huo.

Hata hivyo, huenda Marekani isikubaliane na takwa hilo hasa ikizingatiwa, mwaka uliopita, Rais Trump aliiondoa nchi yake kwenye makubaliano ya Paris ya mwaka 2015 kuhusu mabadiliko ya tabia nchi. ***DW***

# Kansela Angela Merkel anaumwa?

**BERLIN, Ujerumani**

KANSELA wa Ujerumani Angela Merkel, alionekana akitetemeka kwa mara nyingine tena mjini Berlin Alhamisi wiki hii wakati wa hafla ya kumwapisha Waziri wa Sheria.

Kiongozi huyo alitetemeka mjini Berlin, siku nane baada ya kufanya hivyo. Video inayoonyesha Merkel mwenye miaka 64, akijikunyata kwa mikono yake huku mwili wake ukitetemeka.

Hata hivyo, badaa ya dakika chache alirejea katika hali ya kawaida na akasalimiana kwa mikono na Waziri wa Sheria wa Ujerumani Christine Lambrecht.

Alipewa glasi ya maji ya kunywa, lakini hakuyanywa. Katika tukio la awali Merkel alisema kutetemeka kwa mwili kulitokana na upungufu wa maji mwilini.

Baadaye baada ya tukio hilo, aliondoka kuelekea katika mkutano wa G20 nchini Japan mchana kama ilivyokuwa imepangwa.

Mambo yote yanaendelea kama ilivyopangwa. Kansela wa shirikisho yuko salama," alisema msemaji wake Steffen Seibert.

Shirika la Habari la Ujerumani DPA lilisema kuwa licha ya kipindi cha joto nchini humo, joto lilikuwa limepungua wakati wa hafla iliyofanyika katika kasri la Bellevue, ambako Rais Frank-Walter Steinmeier alikuwa akimtangaza Waziri mpya wa Sheria Christine Lambrecht.

Mara ya mwisho, Merkel alitetemeka alipokuwa amesimama pembeni ya Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky chini ya jua. Alisema alijihisi vizuri baada ya kunywa maji.

Siku ya Alhamisi alihudhuria kuapishwa kwa Bi Lambrecht bungeni (Bundestag) kwa muda mfupi -na baadaye akaondoka.

Atakaporejea kutoka Japan, Merkel atakabiliwa na mazungumzo magumu mjini Brussels wakati ambapo yeye na viongozi wengine wa Muungano wa Ulaya watakuwa wakimtafuta mgombea wa urais wa Tume ya Muungano wa Ulaya atakayechukua nafasi ya Jean-Claude Juncker.

Duru za serikali zimeviambia vyombo vya habari vya Ujerumani kuwa hakukuwa na cha kuhofia na alipokuwa anaondoka kuelekea Osaka, msemaji wake alituma ujumbe wa tweeter kwamba" mazungumzo ya ushirikiano yamepangwa na wakuu wengine wa serikali na nchi".

**BBC**

# HADITHI

# Jumba Jekundu-7

WASWAHILI wana msemo wao unaosema kuwa ufukara ni jereha la ulimwengu. Wakiwa na maana, mtu fukara mara nyingi hukutana na mitihani mikubwa duniani, ambayo mingi husababishwa na baadhi ya binadamu wengine wenye vipato kwa kuwaona hawana thamani na hawahitajiki kuwa na kitu chochote cha thamani.
Kijana anayetoka kwenye familia duni Kadili, anatokea kupendwa na msichana mrembo anayetoka kwenye familia ya kitajiri, Edina.
Lakini kitendo hicho kinamsababishia kijana huyo matatizo makubwa ambayo hajawahi kuyapata katika maisha yake, kiasi cha maisha yake kuwa hatarini. Fuatilia mkasa huu wa aina yake.

**Na Adam Fungamwango ,**

**(0716 350534)**




HAKUKUWA na mti wowote walioona maeneo hayo ambayo yangeweza kutoa kivuli cha binadamu au kiumbe hai yoyote yule kujipumzisha kutokana na jua kali.

Kutokana na hali hiyo, mama Kadili alikuwa ametandika mkeka pembeni kidogo ya nyumba yake ambako jua limeelekea na kufanya kivuli kidogo cha nyumba.

Kivuli hicho kidogo ndicho kilichomfanya mama huyo kutoa mkeka wake na kujiweka hapo akisuka ukili.

"He bibi wewe naona mwaka huu umeng'ang'ania tu kusuka ukili na kutoa mikeka, au ndiyo unataka kumtunza mkwe wetu?" Ilikuwa ni sauti ya mama Gombea ambaye alikuwa amefika hapo bila ya kuonekana na mama Kadili, kabla ya kuisikia sauti.

"Na wewe nawe mama Gombea, hii mikeka mimi mwenzako nauza ndiyo nipate pesa ya mchezo na ninavyokwambia wiki ijayo zamu yangu."

"Ai mwenzangu mimi nilijua ndiyo michango ya harusi ishaanza hivyo."

Mama Kadili alijua yale maneno anayosema shoga yake, basi kuna kitu anataka kusema. Na hiyo inatokana na tabia yake ya umbea mtaani hapo.

"Basi ndiyo ushapata jambo lako huko, unataka kunitupia hapa, haya lete hicho ulichokileta," mama Kadili.

Mama Gombea aliamua kujibana hapo hapo kwenye mkeka wa mwenzake.

"Kwanza yupo?"

"Nani?"

"Kadili."

"Hayupo."

"Siku ile si nilikwambia kama mwanao ana msichana, tena wa kitajiri."

"Nakumbuka na nikakwambia ndiyo maana siku hizi amebadilika kama hana raha vile."

"Basi kumbe huyo msichana ampata kwenye disco huko wanakokwenda, ni kweli yupo anaitwa Edina na anakaa Masaki."

"Wewe mama Gombea hizi habari huwa unazipata wapi?"

"Mimi si ndiyo mbea wenu wa mtaa, sasa unashangaa nini?" Naye aliuliza.

"Lakini naona siku hizi Kadili ana furaha siyo kama wiki zile zilizopita."

"Labda mambo yameshakuwa mazuri, kwa hiyo jiandae tu shoga yangu."

"Lakini mbona mwanangu hana sana mambo ya macho juu juu kwa wasichana navyomuona?"

"Alikuwa hajapata dada wee."

"Haya tutayaona, mimi nipo," mama Kadili aliongea kwa sauti ya chini.

"Sasa shoga si unaikumbuka ile shughuli niliyokwambia siku ile?" Aliuliza mama Gombea huku akimkazia uso mwenzake.

"Naikumbuka, si wiki ijayo?" Mama Kadili naye alijibu kwa swali.

"Basi mwaya, ndiyo nakwenda kwa mama Mtupeni, ana mpwa wake ana kikundi chake cha matarumbeta, nataka aongee nao ili bei ipungue mwaya."

"Itanogaje shughuli ya mtoto wa shangazi yako?"

"We acha mama Kadili, shangazi mwenyewe atashangaa, maana hii kampani yetu hapa ikitoka kwenda kule itakuwa balaa tupu, hatutoshikika, hapa mimi mwaya, hapa wewe mama Kadili, hapa kuna vichaa kina mama Sufiani, Suzana, na yule msichana wa kule karibu na gengeni, maana yule ngoma ikimkolea hachelewi hata kusasambua." Alikuwa akiongea huku akiigiza kucheza bila muziki, mama Kadili akimuangalia huku akitabasamu.

"Mama Mwenda haendi?"

"Mwaya we, amepigwa marufuku na mumewe, mumewe ana wivu hatari, kuna siku pale pale tu mitaa ya nyumbani kulikuwa na rusha roho alitoka kwake kuja kuangalia tu mara moja, alifuatwa hapo hapo akapigwa makofi mbele za watu. Ana hamu tena? Bibi yule ukimuona ametoka kwenda shughuli basi za ndugu zake, maana hapo sasa mumewe hana ujanja, au ndugu za mumewe." Umbea wa mama Gombea ulizidi kushamiri. Alikuwa akiongea huku ameshika kiuno.

"Sasa na yeye akimcheza mtoto wake Bahati itakuwaje, maana karibuni awe mwari yule msichana." Aliuliza Mama kadili.

"Watakuja ndugu zake na za mumewe, mimi siinui mguu wangu huu kwenda kwa mtu ambaye hana kampani."

"Shikamoo" Ilikuwa ni sauti mpya kwenye mazungumzo yao na iliwafanya kushtuka kidogo na kugeuza shingo zao.

Walikutana na sura ya Kadili akiwa ametoka matembezini. 'Marahaba" Aliitikia mama Gombea ambaye alikuwa yeye ndiye mlengwa wa salamu ile.

Wakati amewapa kisogo anaingia ndani, mama Gombea akimfinya jicho mwenzake na kumwambia mwenzake kwa sauti ya chini.

"Eeh mwenzangu, ngoja niondoke mie."

"Haya mama Gombea karibu."

"Haya ila usisahau sare yetu ni ile ile ya bluu."

****************************************

Baada ya mazungumzo ya kawaida na mama yake, Kadili aliimuomba tena ruhusa mama yake kuwa wikiendi anataka tena kwenda disco.

"Mmh, mwanangu huko disco kutakuwa disco, maana tangu mara ya kwanza nilipokuruhusu kwenda kumekunogea kama vile wanagawa biriani bure, hebu nieleze kuna nini haswa?"

"Mama si tunakwenda tu na Meze kufurahi na kucheza."

"Ndiyo kila wiki, siyo kama zamani mlikuwa mnaweza kwenda kwa mwezi mara moja, au miezi miwili mara tatu, lakini sasa kila wiki vipi?"

Kadili alishtukia sababu ya maswali hayo. Awali alianza kuwa na wasiwasi na mama yake alipomtuhumu kuwa hakuwa kwenye hali yake ya kawaida, lakini sasa anaonekana anauliza sana maswali ya disco kuna nini?

"Inawezekana kuna kitu anakifahamu." Alijiambia.

"Inawezekana mama akawa anafahamu habari za Edina kweli? Nani anamwambia? Na kitu gani anachoambiwa?" Haya ni maswali aliyokuwa akijiuliza.

Kwa mbali alianza kuhisi kuwa kuna mtu anavujisha siri wakati anaongea na Meze.

Anachojua yeye ni kwamba hakuna mtu yeyote anayeongea naye zaidi ya rafiki yake kipenzi Meze.

"Ni Meze ndiye anavujisha siri? Hapana". Alijiuliza na kujijibu mwenyewe.

Kwa mbali alianza kuhisi kuwa kuna mtu huwa anasikiliza maongezi yao anapokuwa dukani na rafiki yake.

Wakati anawasili nyumbani alikutana na mama mmoja, anaitwa mama Gombea.

Huyu ni mama anayesifika kwa umbea, kutoka maneno huku kupeleka kwingine.

"Inawezekana ni mama Gombea." Alijiambia.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### ELIMU/ MASOMO


**NAFASI ZA MASOMO,** Chuo cha Uuguzi na Ukunga MASSANA kilichopo dar es Salaam, Mbezi Beach Goba Road. Kinatangaza nafasi za masomo kwa ngazi ya Diploma na cheti yatakayoanza mwezi wa September 2019. Njoo tukujazie Form Kupitia Mtandao wa Nacte: 0713 321260/0769 666880


## NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA



### CHETI KIMEPOTEA



**SHABANI A. MNANGO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.3225/314** kilichotolewa na CHARAMBE SEKONDARI mwaka 2017. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/MBA/RB/88428/2019.**

215300302


### KUPOTEA KWA VYETI



**Selemani Omari** anatangaza kupotea kwa vyeti vifuatavyo cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.328/129** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 1982 katika shule ya Sekondari Mawenzi,cheti cha kidato cha sita chenye index namba S.350/608 kilichotolewa pia na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 1985 katika Shinyanga Commercial Institute na Leaving Certificate kutoka chuo cha University of Dar es Salaam Reg namba 4604/T85 kilichotolewa mwaka 1989. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. **Polisi Taarifa: KW/RB/4205/19**

115299802

### KUPOTEA KWA CHETI



**Lwitiko G. Mwakasata** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye **index namb S.2279-0052** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2009 katika Shule ya Sekondari N'gamba. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **MBZ/RB/2313/2017**

115299702

### SHIRIKA LA BIMA LA ZANZIBAR

**TAARIFA KWA UMMA**

**KUPOTEA KWA KITABU CHA STIKA ZA BIMA**

SHIRIKA LA BIMA LA ZANZIBAR LINATANGAZA KUPOTEA KWA KITABU CHA STIKA ZA BIMA CHENYE NAMBA KUANZIA 9199445 MPAKA 9199500. YEYOTE ATAKAE KIONA ATOE TAARIBA POLISI: **MS/RB/4984/2019**

**AU SIM NAMBA +255 24 2232676 AU TIRA.**

115530102

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
28/06/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya JUMATATU tarehe 01/07/2019 kampuni ya **TARIMO REMI STANSLAUS** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **MTO WA MBU kuelekea LUGALO DAR ES SALAAM,** gari hilo lina namba za usajili: **T.155BJM//T916DCG.**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 17.50**
   **Upana – mita 2.98**
   **Kimo – mita 4.60**
3. Njia itakayotumika **MTO WA MBU hadi LUGALO DAR ES SALAAM** kupitia TANGA, gari litasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

115300402

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Airport Tax Co-operative Society Limited** wanatangaza kupotelewa na kadi halisi ya gari yenye usajili wa namba **T 244 DJX** aina ya **TOYOTA VITZ.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **DAR/OST/RB/35395/2019**

115299602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**Kumb. Na. MADAI NA. 238/2019**

**YAH: SHAURI LA MADAI NA 238/2019**

**MDAI................PUNUNTA'S COMPANY LTD**

**DHIDI YA**

**MDAIWA .......................GISELA ALBINUS**

Unaamriwa na Mahakama ya mwanzo Mjini Mwanza kufika tarehe 03/07/2019 saa 2.00 asubuhi bila kukosa ili kujibu madai tajwa hapo juu. Endapo hutafika mahakamani shauri litasikilizwa na kutolewa uamuzi bila wewe kuwepo.

E.S. Mizana
HAKIMU MKAZI MFAWIDHI
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MWANZA.

115299502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA SUMBAWANGA MKOA WA RUKWA**

**SHAURI LA MAOMBI YA ARDHI NA; 15 LA MWAKA 2019**

**SIMON PETER KIMITI ..............................MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**JOSEPH BALTAZAR KAMEKA ................MJIBU MAOMBI**

**TANGAZO LA WITO WA KUITWA SHAURINI**

Wito huu unatolewa kwa Ndugu JOSEPH BALTAZAR KAMEKA wa S.L.P 147, Sumbawanga, Rukwa kuhudhuria shauri la Maombi ya Ardhi Na. 15 la mwaka 2019 katika Baraza la Ardhi na Nyumba, Wilaya ya Sumbawanga, Mkoa wa Rukwa, siku ya tarehe 30 Julai, 2019 saa 3.00 kamili Asubuhi bila kukosa ambapo shauri hilo limepangwa kusikilizwa mbele ya Mwenyekiti wa Baraza

Kutofika kwako siku ya tarehe 30 Julai, 2019 saa 3.00 kamili Asubuhi kutapelekea shauri hilo kuendekea kusikilizwa upande mmoja

**Imetolewa na:**
**Justina Rwezaura**

115300102

**IN THE DISTRICT DELEGATE MAGISTRATE'S COURT OF DODOMA AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO.. OF 2019**

**In the matter of the Estate of the late RUTH DAUD KOMBA of KIKUYUMISSION within DODOMA CITY**

**AND**

**In the matter of an application for letters of Administration by ADALGOT DAUD KOMBA**

**GENERAL CITATION**

**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN. 369 OF 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioners.

Objections to the grant should be filled on or before the 26 Day of 7 2019.

115300102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM 11**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika Mahakama ya Mwanzo DODOMA MJINI**

**Usimamizi wa mirathi 47/2019**

**Ombi la SHIDA HUSSEIN kuteuliwa Msimamizi wa mirathi Marehemu ADAM MWINYIMVUA KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA TANZANIA BARA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnano tarehe 11/7//2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe 27/6/2019

115300202

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**HOSANA RUGA BALIGE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 532 CHD MITSUBISHI CANTER**. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/OST/RB/88320/2019.**

115300702

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**LINUS CHARLES NYANGALIMA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T.607 AHQ** RANGI YA GREEM.YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU. TAARIFA YA POLISI **MBE/RB/89022/2019**

115300502


*Kwa Habari Motomoto*


*usikose Gazeti lako la*

*Nipashe kila siku*

*Tupigie 0767 223 311*

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi*
*Kwa Bei Poa Tupigie 0767 223 311*


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# CAHILL AGOMBEWA NA ARSENAL, WEST HAM

**LONDON, England**

NAHODHA wa zamani wa Chelsea, Gary Cahill amekuwa akiwaniwa na klabu kadhaa za Ligi Kuu ya England baada ya kuondoka pale Stamford Bridge.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, alitumia misimu nane kwa klabu hiyo ya London Magharibi baada ya kujiunga nayo akitokea Bolton kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni saba.

Akiwa Chelsea amecheza jumla ya mechi 290 katika mashindano yote na kutwaa mataji mawili ya Ligi Kuu, mawili ya Europa, mawili ya FA na moja la Ligi ya Mabingwa Ulaya katika msimu wake wa kwanza na klabu hiyo.

Aliruhusiwa kuondoka kipindi cha majira ya joto, baada ya kushindwa kumshawishi kocha wa zamani wa Chelsea, Maurizio Sarri.

Sky Sports imeripoti kwamba, Cahill sasa anawaniwa na Klabu za Arsenal, West Ham na Crystal Palace.

Arsenal wanamtaka Cahill kwa ajili ya kuimarisha safu yao ya ulinzi ambayo msimu uliopita ilionekana kupwaya.

Hadi sasa Cahill amecheza jumla ya mechi 349 za Ligi Kuu England tangu alipoanza kucheza kwenye ligi hiyo msimu wa 2005/06 na pia ameichezea timu ya Taifa ya England jumla ya mechi 61 kwa kipindi cha miaka nane.




# JUVENTUS YAMRUDISHA BUFFON

**TURIN, Italia**

KLABU ya Juventus imefikia makubaliano na golikipa mkongwe, Gianluigi Buffon ili kurudi pale Turin, baada ya mwaka moja akicheza kule Paris Saint-Germain.

Buffon alijiunga na PSG kwa uhamisho huru kipindi cha majira ya joto kilichopita, baada ya mkataba wake kumalizika akiwa amekaa miaka 17 hapo Bianconeri.

Uhamisho wa Mtaliano huyo ulionekana kama ungeweza kumpa nafasi ya kubeba taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya kwanza, lakini PSG walitolewa na Manchester United hatua ya 16-bora.

Na sasa baada ya mkataba wake wa mwaka mmoja kumalizika na miamba hao wa Ufaransa, Buffon yupo tayari kurudi Juve, huku mwandishi wa michezo wa Italia, Romeo Agresti akiripoti kwamba, pande hizo mbili zimeshafikia makubaliano ya kutia saini ya mwaka mmoja.

Kipa huyo mwenye umri wa miaka 41, ambaye alicheza mechi 25 akiwa na PSG kwenye mashindano yote, atapata mshahara wa euro milioni 1.5 pamoja na bonasi.

"Nina furaha nimepata uzoefu wa kucheza Ufaransa na nimekua. Leo hii naona fahari kurudi katika klabu niliyoanza kuichezea.

"Ningependa kumshuruku Mwenyekiti Nasser Al-Khelaïfi, klabu na wachezaji wote kwa ujumla. Nawatakia kila la heri.

# AC Milan yafungiwa kushiriki Ligi ya Europa

**MILAN, Italia**

AC Milan imeondolewa kushiriki michuano ya Ligi ya Europa kwa msimu wa 2019/20, kwa kukubali adhabu ya kuvunja sheria ya haki sawa ya matumizi ya fedha kwenye usajili.

Sasa Milan hawatacheza michuano hiyo licha ya kufuzu kwa kumaliza nafasi ya tano katika msimamo wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A. Maamuzi hayo yametoka katika Mahakama ya Usuluhishi ya Michezo (CAS), baada ya Milan kukubali kwamba walikiuka sheria hiyo ya Shirikisho la Vyama vya Soka Ulaya (Uefa), miaka miwili iliyopita.

Na wameombwa kuondolewa kwenye mashindano hayo ya pili kwa ukubwa Ulaya kwa ngazi ya klabu ili kupata muda wa kuisahihisha.

Taarifa ya CAS ilisema: "Mahakama ya Usuluhishi wa Michezo (CAS) inatoa taarifa kwamba, kumefikiwa makubaliano kati ya AC Milan na Shirikisho la Vyama vya Soka Ulaya, (Uefa), kuhusu kuvunjwa kwa sheria ya haki sawa ya kifedha kulikofanywa na klabu hiyo ya Italia."

Hivyo, msimu huu Milan haitashiriki kwenye michuano hiyo ikitumikia adhabu yake hiyo.

## HABARI MICHEZO




# MAKAMU RAIS BARCA AMKATAA NEYMAR

**BARCELONA, Hispania**

LICHA ya mshambuliaji wa Paris St-Germain, Neymar kuripotiwa kutaka kurudi Barcelona, lakini Makamu Rais wa Klabu hiyo ya Hispania, Jordi Cardoner amesisitiza kuwa hakuna mawasiliano yoyote yaliyofanyika kati yao na mchezaji huyo.

Nyota huyo wa Brazil amekuwa na wakati mgumu katika Klabu ya PSG tangu alipotua hapo kwa dau lililovunja rekodi ya dunia mwaka 2017.

"Kile ninachoamini ni kwamba Neymar anataka kurudi, Cardoner alisema akinukuliwa na Sky Sports.

"Lakini kusema kwamba tumeanza mikakati ya kutaka kumsainisha hicho ni kitu ambacho si cha kweli."

Kumekuwa na uvumi kuhusu ni klabu gani Neymar atahamia iwapo ataondoka PSG, suala ambalo Cardoner aliulizwa katika mkutano na vyombo vya habari siku ya Alhamisi.

Alikiri kwamba ni wazi alikuwa anataka kurudi Barca, lakini akaongezea kwamba klabu yake haijaamua kuhusu kumrudisha tena mchezaji huyo ama hata kufanya mazungumzo naye.

"Hatusajili mtu yeyote kwa sasa hasa mchezaji huyu ambaye hatujawasiliana naye," alisema.

Uhamisho wa Neymar wa kuelekea PSG mwaka 2017 ulivunja rekodi ya dunia huku klabu hiyo ya Ligue 1 ikilipa dau la pauni milioni 200.

Aliisaidia timu hiyo kushinda mataji kadhaa ya ligi hiyo na kufunga mabao 34 katika mechi 36, lakini kipindi chake katika uwanja huo wa Parc des Princes kiligubikwa na vurugu na kutoelewana na wachezaji wenzake kwenye vyumba vya kubadilishia nguo.

Kulingana na ripoti katika vyombo vya habari vya Hispania, Neymar amejitolea kupunguziwa mshahara kwa euro milioni 12 kila mwaka ili kuweza kurudi katika klabu hiyo.

Antoine Griezmann anatarajiwa kujiunga na klabu hiyo ya Catalunya kutoka Atletico Madrid kwa dau la euro milioni 120, huku Frenkie de Jong akisaini kwa euro milioni 75 kutoka Ajax.

## GUARDIOLA AMTAJA MRITHI WA SILVA MANCHESTER CITY

**MANCHESTER, England**

WAKATI kiungo wa Manchester City, David Silva ametangaza kuondoka klabuni hapo mwishoni mwa msimu ujao, kocha wake, Pep Guardiola amemtaja nyota wa Real Madrid, Isco kuwa ndiye anayefaa kuchukua nafasi yake.

Nafasi ya Isco katika kikosi cha kocha Zinedine Zidane inatazamiwa kupotea zaidi baada ya klabu hiyo kuendelea kuwanunua mastaa wa nguvu kikosini, lakini inaeleweka Guardiola ni shabiki mkubwa wa Isco.

Guardiola amekuwa akivutiwa na uwezo wa Isco tangu wakati alipokuwa akiifundisha Barcelona na kuna uwezekano mkubwa akatoa dau la kumchukua staa huyo wakati huu dau lake likizidi kushuka zaidi Santiago Bernabeu.

Kocha Zidane amemhakikishia namba Isco katika kikosi cha kwanza, hata hivyo Real Madrid itaipa uzito ofa yoyote ambayo itapelekwa kwao.

Hadi sasa Manchester City haijafanya usajili wowote mkubwa unaoweza kushtua na mipango ya Guardiola ni kutoa changamoto zaidi kwenye Ligi ya Mabingwa wa Ulaya msimu ujao.



# Liverpool hawana mpango na Pepe

**PARIS, Ufaransa**

KLABU ya Liverpool imeripotiwa kwamba haina mpango na saini ya nyota wa Lille ya Ufaransa, Nicolas Pepe.

Pepe amekuwa akitajwa kusakwa na klabu vigogo huko Ulaya kufuatia soka la kiwango cha juu aliloonyesha msimu uliopita kwenye Ligue 1.

Manchester United, Arsenal, Manchester City na hata Liverpool kwa awamu tofauti zimeripotiwa kwamba wanafukuzia huduma ya winga huyo raia wa Ivory Coast, ambaye kwa sasa yupo na kikosi cha timu ya taifa kwenye michuano ya Afcon kule Misri.

Hata hivyo, kuna taarifa mpya zinazodai kwamba Lille wamepigiwa simu na kuelezwa kwamba wasiwahesabie Liverpool kwenye mpango wa kumsajili nyota wao huyo kwa sababu wakali hao wa



Anfield hawana tena mpango wa kunasa saini ya Pepe.

Liverpool ndio waliokuwa wakidaiwa kuwa mstari wa mbele kwenye mbio za kunasa saini ya mchezaji huyo, lakini kitendo cha kujitoa kinatoa nafasi kwa wababe wengine kwenda kunasa huduma yake.

Gezeti la Ufaransa la L'Equipe hivi karibuni lilifichua kwamba Inter Milan wameweka mezani ofa ya pauni milioni 72 kwa ajili ya kunasa huduma ya Pepe ili akakipige kwenye kikosi chao huko Serie A msimu ujao.

Pepe ni mmoja wa mastaa ambao hawaonekani kama wataendelea kubaki kwenye timu zao wanazozitumikia kwa sasa kutokana na huduma zao walizoonyesha msimu uliopita kwenye ligi za nchi zao na hivyo kuwindwa na vigogo wa Ulaya kila kona.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# ROONEY: NAITIWA KAZI YA UKOCHA ENGLAND, MLS

●●●Kuna fursa kwangu ya kwenda katika uongozi moja kwa moja, na wakati nitakapotundika...

**Washington, England**

WAYNE Rooney amefunguka kuwa kitendo cha Chelsea cha kutaka kumteua mchezaji mwenza wa England, Frank Lampard kuinoa, kumeinua "matumaini" ya kufanikiwa katika ukocha.

Rooney ameweka wazi kuwa tayari amepokea ofa kibao za ukocha kote England na Ligi Kuu Marekani (MLS), sehemu ambayo bado anacheza soka akiitumikia DC United.

Jumanne wiki hii Rooney aliweka alama ya kumbukumbu ya mwaka mmoja tangu atue MLS akitokea Ligi Kuu ya England, akifunga bao dhidi ya Orlando City kutoka katikati ya uwanja, hilo likiwa ni la 23 kwake katika mechi 40 alizoichezea timu hiyo yenye makazi yake Washington.

Licha ya ukweli kwamba nyota huyo wa zamani wa England ambaye atatimiza miaka 34 Oktoba mwaka huu, bado hajakamilisha kozi yake ya ukocha, tayari kuna mahitaji ya huduma yake.

Alipoulizwa kama ana wazo la kuwa kocha, Rooney aliiambia Sky Sports News: "Ndiyo bila shaka.

"Ninachukua hatua za kupata beji zangu kukamilika na nitakapomaliza kucheza nitaona ni fursa gani zinazotokea. Tayari kuna ofa ambazo zimeletwa, lakini kwa dakika hii bado ninacheza na ninataka kufurahia kucheza, na kisha nitaona ofa gani ni sahihi wakati nitakapomaliza.

"Kuna fursa kwangu ya kwenda katika uongozi moja kwa moja, na wakati nitakapotundika daluga, uamuzi huo utafanywa na lengo la klabu yangu litakuwa la kwanza kwa yote, na matarajio yangu na ni sahihi kwa mimi mwenyewe na kwa timu maalum. "

Baadhi ya wachezaji wa zamani waliocheza pamoja na Rooney kikosi cha England wameanza kufanya safari ya kuhamia kwenye ukocha, na Frank Lampard akijiandaa kupata kazi ya daraja la juu kufuatia kutarajiwa kuteuliwa kuinoa Chelsea.

Scott Parker atainoa Fulham msimu ujao, John Terry alikuwa kocha msaidizi wa Aston Villa wakati wakifanikiwa kupanda Ligi Kuu wakati Steven Gerrard akifurahia msimu mzuri na Rangers - akiongoza kumaliza nafasi ya pili na kurejea kwenye hatua ya Europa League hatua ya makundi.

"Nadhani ni kipaji kwa Frank, lakini pia kwa makinda wa Kiingereza, au wachezaji ambao wamekwisha kumaliza kucheza, kuona timu kubwa kama Chelsea inampa Frank fursa ya kujidhihirisha mwenyewe," Rooney aliongeza.

"Nina uhakika katika hatua fulani katika miaka michache ijayo Steven (Gerrard) atapata fursa hiyo pale Liverpool.

"Scott Parker, John Terry pale Aston Villa - ni nzuri kwangu binafsi, ambaye ninataka kwenda katika uongozi, kuona vijana hawa wanapata fursa na inakupa matumaini kwamba itatokea kwako."

## KWA UFUPI

**SANE BADO WINDO LA BAYERN**

MSHAMBULIAJI wa Manchester City na Ujerumani, Leroy Sane, 23, anabaki kuwa katika mpango wa kwanza wa usajili majira haya ya joto kwa Bayern Munich licha ya kutokuwapo kwa mwendelezo wa kufanyika kwa mazungumzo ya dili hilo hivi karibuni. ***(Sky Sports)***

**FERNANDES ANUKIA MAN UTD**

KOCHA wa Sporting, Marcel Keizer anaamini nafasi ya kumbakiza kiungo Mreno Bruno Fernandes, 24, katika klabu hiyo ni ndogo, na Manchester United ikiwa miongoni mwa klabu zinazovutiwa naye. ***(Record - in Portuguese)***

**RODRIGUEZ AWINDWA ATLETICO**

ATLETICO Madrid inapanga kumfuata kiungo wa Real Madrid, Mcolombia James Rodriguez, wakati huu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, akionekana kuwa ziada hapo Bernabeu. (Cadena SER - in Spanish)

**ARSENAL YAONYWA KWA TIERNEY**

KOCHA wa Celtic, Neil Lennon ameiambia Arsenal watapaswa kulipa "kiasi kikubwa zaidi" cha fedha kama wanataka kuipata huduma ya beki wa kushoto, Mscotland Kieran Tierney, 22. ***(Telegraph)***

**ZAHA AIPELEKA PALACE NICE**

CRYSTAL Palace inajiandaa kutua Nice kuisaka saini ya winga Mfaransa Allan Saint-Maximin, 22, wakati wakijiandaa kumpoteza mshambuliaji wa kimataifa wa Ivory Coast, Wilfried Zaha, 26. ***(Metro)***

**LUKAKU NGUMU KUTUA INTER**

MANCHESTER United inaonekana kama inataka kukataa pendekezo la pauni milioni 62.7 kutoka Inter Milan la kutaka kuinasa saini ya straika Mbelgiji Romelua Lukaku kwa mkopo kwanza na kisha kumnunua baadaye kwa kiasi hicho. ***(Telegraph)***

**BALDE ATAKIWA NA ARSENAL**

ARSENAL inataka kuinasa saini ya mshambuliaji wa Monaco, Keita Balde, 24, baada ya Inter Milan kuamua kuipata jumla huduma ya nyota huyo wa kimataifa wa Senegal. ***(Le 10 Sport - in French)***

**ZAGADOU AIFUNGULIA ARSENAL**

BEKI wa Borussia Dortmund na Ufaransa U-20, Dan-Axel Zagadou, 20, anataka kuachana na klabu hiyo wakati huu akielezwa kuwindwa na Arsenal. ***(Bild, via Mirror)***

**KEAN KUIKATAA EVERTON KWA INTER**

BABA wa straika wa Juventus ambaye anayewindwa na Everton, Moise Kean, 19, ametangaza kuwa Mtaliano huyo "anataka kutua Inter Milan". ***(Mirror)***

**UMTITI APIGIWA HESABU UNITED**

MANCHESTER United inapanga kutaka kumfuata beki wa Barcelona na Ufaransa, Samuel Umtiti, 25. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

**CEBALLOS AGOMA KUONDOKA MADRID**

KIUNGO wa Real Madrid na Hispania, Dani Ceballos hataki kuachana na miamba hiyo ya La Liga licha ya kutokuwa sehemu ya mipango ya kocha Zinedine Zidane. ***(Marca)***

**CITY, UNITED ZAMWANIA ELMKIES**

MANCHESTER City na Manchester United zinashindana katika mbio za kuinasa saini ya kiungo wa Hoffenheim, Muisrael Ilay Elmkies, 19, ambaye anaweza kuzigharimu pauni milioni 2.5. ***(Sun)***

# MAKONDA AMWANGUKIA MAGUFULI KIPIGO STARS

**Na Somoe Ng'itu, CAIRO**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam na Mwenyekiti wa Kamati ya Ushindi ya Timu ya Taifa (Taifa Stars), amemwomba radhi Rais John Magufuli kwa matokeo mabaya ambayo timu hiyo imepata, lakini akieleza kwamba safari ya mafanikio ndio imeanza.

Makonda alisema anaamini Taifa Stars itabadilika na kupata matokeo mazuri katika mechi ya mwisho, baada ya kujifunza mambo mbalimbali kupitia mechi mbili zilizopita dhidi ya Senegal na Harambee Stars ya Kenya.

Makonda alisema pia anawaomba wadau wa soka kuendelea kuishabikia Stars kwa sababu hatua ambayo wamefika ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon) ni ya kujivunia.

"Hili ni jeshi lililokamilika, timu ya ushindi kamwe haikati tamaa," Makonda alisema.

Alisema kiwango kilichoonyeshwa na Stars katika mechi ya kwanza na ya pili ni tofauti, hivyo anaamini katika mchezo dhidi ya Algeria, pia wataonyesha kiwango bora na kuwafurahisha Watanzania.

"Kwenye uwanja wa mpira, lolote linaweza kutokea, nimeyachukulia matokeo haya si kushindwa, ni chachu ya kusonga mbele kama taifa elekea, namwomba rais wangu radhi, kila mmoja alikuwa amejiandaa kushinda, hakuna aliyetegemea tutashindwa," alisema Makonda.

Aliongeza kuwa baada ya mchezo, alikutana na wachezaji ambao kila mmoja alionekana kuumizwa na matokeo ya mchezo huo, ambao ulibadilika baada ya wachezaji wa Harambee Stars kuwachezea faulo za mara kwa mara nyota wa Stars akiwamo Aishi Manula, Simon Msuva, Thomas Ulimwengu huku Erasto Nyoni akitolewa nje baada ya kubanwa na misuli.

"Mbegu ambayo ilikuwa haijapandwa kwa miaka 39, sasa imeota tena, tunatakiwa tuendelee kuwa na umoja, tunatakiwa tuangalie mbele ili taifa letu lifanye vizuri katika mashindano yanayokuja," aliongeza Makonda.

Kiongozi huyo pamoja na wajumbe wenzake wa Kamati ya Ushindi akiwamo Mohammed Nassor, Hersi Saidi, Patrick Kahemele na Philimon Ntalihaja wako jijini hapa wakiendelea kuhamasisha Stars ifanye vema katika mechi za Kundi C.



Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Meja Jenerali Martin Busungu (watatu kushoto), akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya maofisa wa jeshi hilo, manahodha wa timu mbalimbali za jeshi hilo na wachezaji baada ya kukabidhiwa makombe waliyotwaa katika mashindano mbalimbali. Makabidhiano hayo yalifanyika jana Makao Makuu ya JKT, jijini Dar es Salaam. **PICHA: ISAAC KIJOTI**

# Yanga kuvaana na miamba ya Misri, Morocco

**Na Shufaa Lyimo**

YANGA inatarajia kucheza mchezo wa kirafiki na timu kutoka ama Misri, Guinea, Morocco au Afrika kusini katika siku ya 'Wananchi' itakayofanyika kuanzia Julai 21-27, mwaka huu jijini Dar es Salaam ambayo pia itatumika kutangaza wachezaji wao wapya waliowasajili kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu Bara na michuano ya kimataifa, imeelezwa.

Mwenyekiti wa klabu hiyo yenye makao yake makuu mtaa wa Twiga na Jangwani jijini Dar es Salaam, Mshindo Msolla, ndiye aliyetoa kauli hiyo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa na kuongeza kuwa tayari usajili wao umekamilika.

"Tunatarajia kucheza mchezo wa kirafiki kati ya timu hizo nilizozitaja mazungumzo mpaka sasa yanaendelea naamini kila kitu kitakwenda vizuri hivyo mashabiki na wanachama wetu tunawaahidi kufanya makubwa zaidi msimu ujao," alisema Msolla.

Mwenyekiti huyo aliongeza kuwa viongozi waliochaguliwa ndani ya klabu hiyo watawajibika vilivyo ikiwa ni pamoja na kuweka uwazi wa mapato na matumizi sahihi yanayotumika ndani ya klabu hiyo na kuwataka wale wote wanaotengeneza nembo za Yanga visivyo halali, kujisalimisha kabla ya kuchukuliwa hatua kali kisheria.

"Sisi kama viongozi tutawajibika vilivyo ili kutimiza malengo yetu pamoja na kuweka wazi matumizi yote ya fedha tutakayokuwa tunayatumia ili mashabiki na wanachama wetu waweze kujua kile kinachoendelea kwa upande wa matumizi ya pesa," alisema.

Kuhusu suala zima la usajili alisema kamati ya usajili imefanya usajili kwa kufuata maelekezo pamoja na mapendekezo ya kocha wao kutoka DR Congo, Mwinyi Zahera ambaye kwa sasa yupo nchini Misri na timu yao ya taifa kwenye michuano ya fainali za Kombe la Mataifa Afrika (Afcon) 2019 zinazoendelea kwa sasa. "Tumefanya usajili kwa kufuata mapendekezo ya kocha wetu kwa kuongeza nafasi alizokuwa ameziona zina upungufu msimu uliopita, lengo letu ni kuanza kambi mapema kwa ajili ya kujiandaa na mashindano ya kimataifa na msimu ujao wa Ligi Kuu," alisema mwenyekiti huyo.

# JKT yafurika makombe, kuboreshewa viwanja

**Na Shufaa Lyimo**

MKUU wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) , Meja Jenerali Martin Busungu, amewaahidi wachezaji wa michezo yote wanaolichezea jeshi hilo kwenye mashindano mbalimbali, kuwaboreshea viwanja ili waweze kufanya mazoezi kwa ufanisi zaidi na hatimaye kuzidi kulileta sifa jeshi hilo na Tanzania kwa ujumla.

Akizungumza na waandishi wa habari jana Makao Makuu ya Jeshi hilo, Mlalakuwa jijini Dar es Salaam wakati alipokuwa akikabidhiwa vikombe walivyopata kutokana na kushinda mashindano mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwakabidhi zawadi, aliahidi kuboresha viwanja hivyo ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kila mchezaji wa timu ya JKT Queens waliomaliza mikataba yao wanaboreshewa na kuendelea kuichezea timu hiyo.

**"Nawaahidi wachezaji mpaka ifikapo Julai 10, mwaka huu viwanja vyote vitakuwa tayari hivyo naamini changamoto za viwanja hazitakuwapo tena na kuhakikisha utawala unakuwa bora zaidi," alisema Meja Jenerali Busungu.**

Alisema amefurahishwa kuona timu ya Wanawake ya JKT Queens inatwaa tena ubingwa wa Ligi Kuu kwa mwaka wa pili mfululizo na kuwataka kuongeza juhudi zaidi katika mashindano mengine yajayo, ili waweze kuipeperusha vema bendera ya taifa.

Timu hizo zilivuna jumla ya makombe 14 mbali na makombe binafsi ya mchezaji mmoja mmoja kutokana na mashindano mbalimbali waliyoshiriki ndani na nje ya nchi ambapo pia Meja Jenerali Busungu aliwazawadia washindi wote.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Elimu, Michezo na Utamaduni wa JKT, Kanali Joel Meidim, alisema sababu ya timu zao kufika hapa ni kutokana na nidhamu nzuri walizo nazo wachezaji kwa walimu wao ikiwa ni pamoja na kukaa kwenye mazingira mazuri.

Aliwataka wachezaji wote kuongeza morali panpokuwa na mashindano ili wazidi kusonga mbele zaidi pamoja na kujitangaza ndani na nje ya nchi.

"Mpaka hatua hii wachezaji wetu walipofikia na kuweza kupata makombe mbalimbali ni kutokana na juhudi na nidhamu za hali ya juu wanazozionyesha wanapokuwa mchezoni na ninaahidi watafika mbali zaidi," alisema Kanali Joel.

Michezo
Jumamosi Juni 29, 2019
Nipashe



## Rooney: Naitiwa kazi ya ukocha England, MLS

HABARI UK 30

LA PILI...



Nahodha wa Taifa Stars, Mbwana Samatta, akishangilia baada ya kuifungia timu yake bao la pili wakati ikichapwa 3-2 na Harambee Stars kwenye mechi ya Kundi C ya fainali ya michuano ya Afcon 2019 iliyopigwa Uwanja wa 30 June jijini Cairo, Misri juzi. **PICHA: SOMOE NG'ITU**

# WANYAMA ACHAMBUA UDHAIFU WA TAIFA STARS

## ●●●Amunike atoa yake, Waziri Mkuu amshushia sifa Manula akiitaka TFF, wizara...

**Na Somoe Ng'itu, CAIRO**

NAHODHA wa timu ya Taifa ya Kenya (Harambee Stars), Victor Wanyama, amesema vitendo vya kupoteza muda na kukosa uzoefu kwa wachezaji wa Taifa Stars ndivyo vilivyowasaidia wao kupata ushindi wa mabao 3-2 katika mechi ya michuano ya Afcon ya Kundi C dhidi ya Taifa Stars iliyochezwa juzi kwenye Uwanja wa 30 June jijini hapa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Wanyama, alisema licha ya timu yao kuwa nyuma, hawakukata tamaa na kukumbushana kuendelea kupambana kwa sababu waliamini wataibuka na ushindi katika mchezo huo.

Wanyama alisema pia wanaamini kiwango cha Harambee Stars ni cha juu zaidi ukilinganisha na cha wapinzani wao Taifa Stars.

"Hatukuwa na wasiwasi, wao walionekana wamepaniki, walianza kujiangusha ili kupoteza muda, sisi tulisema tunaweza, tunacheza kwa nguvu na hata ingekuwa dakika 100, tungepambana bila kuchoka," alisema Wanyama ambaye anacheza katika Klabu ya Tottenham Spurs ya England.

Naye Michael Olunga, alisema juzi ilikuwa ni siku ya furaha sana kwake kwa Wakenya kupata ushindi ambao umewasaidia kuwapa nguvu kuelekea mchezo wa mwisho.

Olunga alisema kwamba walijiandaa kufanya vema katika fainali hizi, na wanaamini ushindi wa juzi umeongeza morali ya kufanya vizuri katika mchezo unaofuata.

Lakini baada ya kupoteza mechi ya pili mfululizo kwenye michuano hiyo, Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Mnigeria Emmanuel Amunike, ameweka wazi kuwa kikosi chake hakikuwa na uwezo wa kupambana na kushindana katika mechi hizo za Afcon 2019 zinazoendelea nchini Misri.

Hata hivyo, kauli hiyo ya Amunike inapingana na ile aliyoitoa kabla ya kuwavaa Harambee Stars, ambayo alisema wamejiandaa kupata ushindi, na kueleza kwamba timu hizi zinajuana na zinazungumza lugha moja ya Kiswahili.

Taifa Stars ilifungwa mabao 2-0 na Senegal na juzi usiku ikakubali kichapo kingine cha mabao 3-2 kutoka kwa majirani zao Harambee Stars ya Kenya, na sasa itamaliza mechi yake ya mwisho ya kukamilisha ratiba dhidi ya Algeria itakayochezwa Jumatatu.

Akizungumza na gazeti hili baada ya mechi hiyo kumalizika, Amunike alisema kuwa kikosi chake hakikuwa na uwezo wa kushindana kama zilivyo timu nyingine zinazoshiriki fainali hizi kwa sababu wachezaji wake hawana uzoefu na mashindano ya mwaka huu, kwao ameyachukulia ni sehemu ya kuja kujifunza.

"Ukweli ni kuwa hatukuwa tumejiandaa kushindana, huo ndio ukweli wenyewe, kama huwezi kujilinda, lazima uadhibiwe, hicho ndicho kilichotokea wakati Kenya wanasawazisha bao la pili, ni vitu ambavyo tulikuwa tunavifanyia mazoezi," alisema Amunike na kuongeza.

"Wachezaji wanahitaji kupata uzoefu, ili waweze kushindana katika ngazi za kimataifa, ukweli ni kwamba hatukuwa katika nafasi ya kushindana, hatukuwa tayari kupambana, tunachotakiwa kukifanya ni kurudi nyuma na kujipanga kuiimarisha timu hii, naamini katika mashindano yajayo, tutakuja tukiwa bora zaidi."

Naye nahodha wa Taifa Stars, Mbwana Samatta, alisema kuwa wameumia sana kwa matokeo ambayo wamepata katika mchezo huo, ambao awali walionekana uko upande wao.

"Tumeumia sana, mechi ilikuwa upande wetu kabisa, tulianza vizuri na tuliamini itamalizika vizuri, ila mwisho wa siku ni lazima ukubaliane na matokeo ya mpira, " alisema kwa kifupi nahodha huyo ambaye kwa sasa anawindwa na klabu zinazoshiriki Ligi Kuu England ikiwamo Cardiff.

### WAZIRI MKUU AFUNGUKA

**Katika hatua nyingine, Augusta Njoji kutoka Dodoma,** anaripoti kuwa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo pamoja na Taasisi zake ikiwamo Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), limetakiwa kutumia matokeo ya Taifa Stars iliyoyapata katika Afcon kujitathmini na kuja na mipango bora zaidi ya kuwekeza kwenye soka la vijana na walimu.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alipokuwa akitoa hotuba ya kuahirisha Mkutano wa Bunge la Bajeti jijini Dodoma.

Majaliwa aliwataka pia wachezaji, benchi la ufundi na wadau wote wa mpira wa miguu nchini kutumia matokeo hayo kujifunza, kujitathmini na kuja na mipango bora zaidi ya kuendeleza soka hususan kwa kuwekeza kwenye soka la vijana na walimu.

Katika hotuba yake, waziri mkuu alipongeza timu hiyo na kudai kuwa imeonyesha ubora.

"Taifa Stars wanastahili pongezi kwa kujitahidi kuwadhibiti Senegal licha ya kupoteza kwa mabao mawili, kuonyesha ubora wa mchezo dhidi ya Kenya licha ya kupoteza pia," alisema.

Hata hivyo, alimpongeza Mlinda Mlango Aishi Manula kwa kazi nzuri, uwezo mzuri aliouonyesha wa kuzuia mashambulizi mengi ya hatari hakika anastahili kupongezwa.

## Wabrazil wafurika Simba wa3 atua

**Na Mwandishi Wetu**

SIMBA sasa haitaki mchezo! Hivyo ndivyo unavyoweza kusema baada ya kushusha beki mwingine kutoka Brazil, Tairone Santos da Silva ambaye ameanguka wino kwa mkataba wa miaka miwili kujiunga na mabingwa hao wa Tanzania Bara.

Santos da Silva, 30, anajiunga na Simba akitokea klabu ya Atletico Cearense FC inayocheza Ligi Daraja la Nne nchini Brazil, maarufu kama Serie D. Santos da Silva anakuwa Mbrazil wa tatu kusaini kuichezea Simba baada ya beki Gerson Fraga Vieira kutoka Klabu ya ATK ya Ligi Kuu ya India na mshambuliaji Wilker Henrique da Silva kutoka Bragantino ya Ligi ya Brazil.

"Kazi ya kuimarisha kikosi cha Mabingwa wa nchi inaendelea kama kawaida, beki Tairone Santos da Silva (30) amesaini mkataba wa miaka miwili kuchezea Msimbazi. @tairone89 amejiunga na klabu yetu akitokea ya Atlético Cearense FC ya nchini kwao Brazil," ilisomeka taarifa ya Simba jana. Mbali na Wabrazil hao, Simba pia imewasainisha kipa Beno Kakolanya kutoka Yanga, beki Kennedy Wilson Juma kutoka Singida United za nyumbani, kiungo Msudan Sharaf Eldin Shiboub Ali Abdalrahman na Vieira na Henrique da Silva kutoka Al Hilal ya kwao.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042